IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 2

Aprili- Mei- Juni 2024

# HabariNjema

## KILA SIKU

**BURE**
HALIUZWI
CHAPISHO HILI LIMELIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI LISAMBAZWE BURE

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO **HABARINJEMA** ITOKAYO NCHI YA MBALI. (MITHALI 25:25).

Uebert & BeBe
ANGEL



## UEBERT & BEBE ANGEL

Wakiwa na miaka mingi ya kufanya huduma, Uebert na BeBe Angel ni watangulizi na sauti zinazoongoza katika kutangaza Habari Njema ya neema ya Mungu (Euaggelion) na unabii duniani kote. Kwa pamoja ni waandishi bora wa vitabu vinavyouza sana kama vile Spiritual Warfare, Intimacy, Prayer Banks, Supernatural Power of The Believer, n.k. Uebert na BeBe Angel ni wazungumzaji wa mikutano wanaotafutwa sana kimataifa na kama viongozi wa kimataifa, wanaheshimiwa sana kwa maono yao, ubunifu, na ujasiri. Kama waanzilishi wa Kanisa la Good News Church (Spirit Embassy) na wanaokalia ofisi ya kinabii wameathiri maisha ya mamilioni ulimwenguni kote kupitia shauku yao ya kuvuna nafsi kwa kuleta ufunuo wa Habari Njema ya neema ya Mungu (Euaggelion).



**Ufunuo 3:20**
**Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.**

Somo moja kuu ambalo ningependa kila mtu aondoke nalo kwenye mstari huu ni kwamba Bwana Yesu Kristo HABISHI hodi mlangoni mwa Kanisa; Anabisha hodi moyoni mwako.

Mstari huo hausemi ikiwa Kanisa litafungua milango yake kwa maongozi ya Mungu; wito huu ni kwa watu binafsi. Watu binafsi ndio wanaofungua milango ya mioyo yao. Kuwa mshirika wa kanisa au cheo havikuhakikishii uhusiano na Mungu. Kwa hiyo njia pekee ya Kanisa la Mungu kukaa sawa ni kwa kila asomaye kukaa sawa. Kumbuka kwamba Kanisa si jengo; kanisa ni wewe na mimi. Katika mwaka huu wa maziwa na asali, acha ufunuo huu uwe kweli katika maisha yako katika Jina la Yesu!

Fungua mlango wa moyo wako. Anabisha hodi!

## UKIRI WA KINABII

**Moyo wangu unaangazia jambo zuri na uko wazi kwa Baba yangu wa Mbinguni kukaa na kuishi. Niko tayari kwa mahusiano Naye ya kina zaidi kuanzia sasa. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 10:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Waamuzi 6-7



**Yakobo 2:17**
**Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake.**

Hebu fikiria kwa sekunde moja jinsi mzazi atakavyofanya yote ili kumpatia mtoto wao kilicho bora zaidi, ili tu mtoto huyo asiishi kama ombaomba kana kwamba hana vitu hata kidogo. Kwa bahati mbaya, hali hii ni kweli kwa watoto Mungu walio wengi. Wanaishi kama maskini, ilihali damu ya kifalme inatiririka kwenye mishipa yao ya kifalme.

Unaona, unapopokea Neno kuhusu ustawi wako, afya, au biashara yako, kwa mfano, ni muhimu kuliunga mkono kwa matendo sahihi. Bila kuchukua hatua, hali yako inaweza kubaki vilevile, na ukawa mtu aliyekata tamaa.

Elewa kwamba Neno lina uwezo wa kubadilisha hali yako NA tambua mwito wa kutenda unaoambatana nalo na uitikie mara moja. Cheza kuendana na muito wake! Usisite au kusubiri. Kwa kutenda kwa imani, unajiweka mwenyewe kwenye kufurahia miujiza kila siku.

## UKIRI WA KINABII

**Ninatabiri ya kwamba nitaiamini mpaka nitaifanya katika Jina la Yesu! Nina imani kwamba Maziwa na asali vitakuwa sehemu yangu katika Jina la Yesu! Haleluya.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 8:7

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waamuzi 8-9



**2 Timotheo 2:1**
**Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu.**

Jambo moja Wakristo wengi hawatambui ni kwamba neema inakutofautisha katika ulimwengu; inakutenga kwenye utukufu na ubora. Unakuwa kichwa juu ya wengine, muasisi, mvunja rekodi na mvunja vikwazo! Hakuna kitu kabisa katika ulimwengu huu, iwe ni umaarufu au utajiri au kuwa na uhusiano bora zaidi, ambacho kinaweza kulinganishwa na kile ambacho neema ya Bwana Yesu Kristo imekupatia.

Kuwa hodari katika neema ya Mungu, kama maandiko ya leo yanavyosema, ni kuenenda katika utimilifu wa neema yake, yaani, kuwa na ufahamu kamili kwamba ni neema ile ile na si uwezo wako mwenyewe unaokufanya kuwa bingwa. Kwa wewe kuwa mzao wa Ibrahimu, neema ya mafanikio inafanya kazi ndani yako. Neema hiyo inakuweka mbele zaidi na kukuweka katika nafasi ya mafanikio katika kila nyanja. Tumia neema hii mwaka huu wa maziwa na asali!

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu ni udhihirisho wa ubora na ukamilifu ninapotembea kwa nguvu katika neema iliyozidishwa, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 6:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waamuzi 10-12



GoodNews DAILY



**Mwanzo 26:12**
**Isaka akapanda mbegu katika nchi ile, akapata mwaka ule vipimo mia kwa kimoja; BWANA akambariki.**

Sasa, ili tu kutoa muktadha kidogo kwa andiko hilo hapo juu, kulikuwa na njaa kubwa katika nchi wakati Isaka alipopanda. Kulikuwa pia na ukame kwa miaka mingi, na kustahimili haikuwa jambo rahisi. Sasa hebu wazia jinsi Mungu anavyomwambia Isaka kwamba atambariki katikati ya haya yote. Hakukuwa na mvua; kila kitu kuanzia utabiri wa hali ya hewa hadi uchumi ulionekana kuwa mbaya sana, hata hivyo Isaka aliendа na kile ambacho Mungu alisema bila kuhojihoji. Inashangaza jinsi alipata mara mia wakati kila mtu alikuwa chini na patupu? Hapana! Hivi ndivyo inavyotokea unapomwamini Mungu.

Hivi sasa, mtu anasoma hili na kujitayarisha kwa kile kinachoonekana kama siku isiyowezekana mbele. Sikiliza, una Neno la Mungu juu ya afya kamilifu, fedha kamilifu, familia kamilifu, kila kitu kamilifu ! Hata pawe na ripoti mbaya katika nchi, simama kwenye Neno la Mungu, na utaona zaidi ya baraka ya mara mia moja!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaamini na kusimama kwenye Neno la Mungu katika kufanikiwa kwenye kila jambo ninalofanya leo bila kuhoji! Asante Bwana kwa maziwa na asali, ambazo ni alama za mafanikio yangu katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 10:22

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waamuzi 13-15



**Waefeso 1:4**
**kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo;**

Tuna Baba wa ajabu kama nini! Fikiria hili kwa sekunde. Upendo wa kina sana hata anatuchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu wetu alitaka tuokolewe, si baada ya mwanadamu kuumbwa wala baada ya mwanadamu kuanguka, bali "kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Akina kaka na akina dada, tuko uso kwa uso na siri nzito lakini iliyo wazi. Kabla hata ya ulimwengu kuanzishwa, wanadamu walionekana kwa Mungu kama waliopotea. Hata hivyo mpango wa wokovu na maelezo yake yalipangwa tangu umilele uliopita. Alichotaka Mungu ni kutotenganishwa kamwe na uumbaji wake mpendwa.

Ndugu, ninyi ni watakatifu na hamna lawama mbele za Baba kwa sababu ya mstari huo hapo juu! Alichukua jukumu kwa ajili ya dhambi zako, na huu ni ujumbe wa Injili, euaggélion , karibia njema sana kuwa Habari Njema ya kweli tunayohubiri, haleluya!

Si ajabu anatuita sisi wenye haki wake, waliohesabiwa haki, kumaanisha kwamba hatuwezi kushtakiwa kwa dhambi kwa sababu sio tu kwamba sisi ni wenye haki, bali pia tumekuwa haki ya Mungu katika Kristo Yesu. Umechaguliwa . Toka leo ukiwa umeinua kichwa juu kwa kulijua hilo tu!

## UKIRI WA KINABII

**Sishindwi leo wala siku yoyote kwa sababu nimechaguliwa! Chochote ninachofanya leo kitaleta matokeo chanya kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waamuzi 16-18



**Mithali 15:4**
**Ulimi safi ni mti wa uzima, bali ukorofi wa ulimi huvunja moyo.**

Neno 'vunja' katika mstari wa leo ni sheber katika Kiebrania. Inamaanisha kuvunja, kukisagasaga au kuponda kitu. Sasa, ukibadilisha neno vunja na ufafanuzi huu, unaweza kuona kwamba maneno mabaya yanaweza kuwa adui mkubwa, kuponda au kuvunja maisha yako na wapendwa wako hivi sasa! Ikiwa kuna uvunjaji kwenye jengo, ina maana adui ameingia katika eneo hilo, na hakuna mtu anayependa wavamizi!

Ufalme wa Mungu, ambao sisi ni mali yake, ni Ufalme wa maneno. Tunaishi, tunaendesha na kutawala kwa maneno. Yote ni kuhusu kile unachosema. Ukiongea sawa, maisha yako yatakuwa sawa. Ikiwa unazungumza vibaya, maisha yako pia yatakuwa mabaya. Katika Kitabu cha Mwanzo, Mungu aliitwa Sauti. "Sauti ya BWANA Mungu akitembea bustanini wakati wa jua kupunga" (Mwanzo 3:8). Sauti si kitu bila maneno. Unapoelewa hili, hutawahi kusema maneno matupu, mabaya. Utatumia maneno kwa usahihi. Utazungumza tu maneno ya baraka, maneno yatoayo uzima na maneno yanayothibitisha maisha ya maziwa na asali.

Anza leo!

## UKIRI WA KINABII

**Kwa uwezo wa ulimi wangu, ninatabiri yaliyo bora tu katika maisha yangu, familia yangu, jamii yangu, taifa langu na mataifa ya ulimwengu. Nguvu na uzima ni vyangu katika Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 18:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Waamuzi 19-21



**Mathayo 5:48**
**Basi ninyi iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.**

"Hakuna mtu mkamilifu!"
Ni mara ngapi umesikia usemi huo katika maisha yako yote? Ikiwa wewe ni kama mimi, inaweza kuwa mara nyingi. Kutoka kwenye uwanja wa michezo hadi kwenye chumba cha mikutano, na hata kwenye mimbari, uwongo huu umejidhihirisha kwa uthabiti. Ukithubutu kutamka maneno "Mimi ni mkamilifu, " watu wanaanza kukuita mwenye kiburi. Hilo ni kosa!

Biblia inasema katika mstari mkuu wa leo, "Iweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu. Neno 'kamilifu' linatokana na neno la Kigiriki téleios , ambalo linamaanisha mtu mzima katika ukomavu, asiye na lawama, asiye na mawaa; kutotaka chochote; ukamilifu. Inarejelea kuupima moyo wako kwa moyo wa Mungu; na njia ya kufanya hivyo ni kupitia Neno. Hii ina maana kwamba unafanya mambo jinsi Mungu angetaka uyafanye; unaruhusu moyo wako uwe kama wa Mungu. Unafikiri, unapenda, na kusamehe kama Mungu anavyofanya kwa sababu una moyo Wake.

Akina kaka na dada, Mungu hatatutaka tufanye kitu ambacho anajua hatuwezi kufanya . Ikiwa anadai ukamilifu kutoka kwetu duniani, inamaanisha kuwa inawezekana.

Ukamilishwe katika yote unayofanya kuanzia sasa, katika Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Maneno, mawazo na matendo yangu ni kamilifu kuanzia leo! Ninatamka maziwa na asali katika kila ninachogusa leo kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wakolosai 1:22

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Ruthu



**2 Wakorintho 5:17**
**Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! Yamekuwa mapya.**

Wakristo wengi wanafikiri mabadiliko haya ni yale yatakayotokea Mbinguni au katika ulimwengu wa roho mahali fulani; tayari yameshatokea! Bwana Yesu Kristo alikuja kutupa uzima wa Ki-Ungu, uzima unaotufanya kuwa wana wa Mungu. Unaona, kuzaliwa mara ya pili haimaanishi una maisha au asili mbili; unao mmoja tu, na huo ni uzima wa namna ya Ki-Mungu, uzima wa Ki-Ungu.

Sasa, angalia maneno "kiumbe kipya"; inaashiria kitu ambacho hakijulikani; ni kipya au hata "ajabu." Wewe na mimi ni spishi mpya, kiumbe ambacho hakijawahi kuwepo, aina mpya ya mtu! Unapokuja kwenye utambuzi huu na kuelewa kwamba ulicho nacho si mchanganyiko wa asili ya Ki-Mungu na ya Kibinadamu, utakoma kutoka katika kupambana ili kuishi sawa, na utajikuta unatimiza mapenzi ya Mungu kwenye maisha yako kwa utukufu kutoka kwenye nafasi ya pumziko. Kuanzia leo, tembea katika mtazamo wa Kristo; tembea katika upya huu. Maisha mapya ndani yako, maisha mapya katika kampuni au biashara yako, watoto wako au chochote kinachokuhusu.

## UKIRI WA KINABII

**Tazama, mimi ni mtu mpya! Nina uwezo wa kushinda mambo yote hasi kutoka mazingira yanayonizunguka, na ninatangaza hivi ndivyo ilivyo sasa hivi, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 1-3



**Wafilipi 3:20**
**Kwa maana wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo.**

Je! unajua Mbinguni ni nchi kama nchi nyingine yoyote, iliyo kamili na serikali na raia ndani yake? Sasa, kama vile nchi yoyote, kuna njia ambazo unaweza kupata kuingia kupitia mipaka yake, yaani uraia au kuingia kwa visa. Bila vigezo hivyo hakuna kufikika. Ndivyo ilivyo na Mbinguni.

Mbingu ni kwa ajili ya viumbe vya mbinguni, wale ambao wana maisha ya mbinguni wakiwa hapa Dunia. Wale ambao wameyatoa maisha yao kabisa kwa Bwana. Hakuna anayeweza kwenda Mbinguni bila kuwa na maisha ya mbinguni. Lazima umiliki hili kabla ya kupewa idhini ya kuingia. Kumbuka, wewe si mtu wa udongoni; wewe ni wa mbinguni. Hebu hii iwe ni mtazamo wako na namna ya maisha. Kila mara, tangaza, "Mimi ni raia wa Mbinguni." Hiyo ndiyo Injili ya Bwana Yesu Kristo; Alikuja kukufanya kuwa raia na kukuwezesha kuingia katika nchi iliyo bora zaidi, Mbinguni!

## UKIRI WA KINABII

**Siko chini ya upotovu na uvutano mbaya wa ulimwengu huu wa sasa. Mimi ni raia wa Mbinguni, na hilo linatatua kila tatizo kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 12:22

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 4-8



**Kumbukumbu la Torati 30:19**
**Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana ;**

Mungu ni muungwana . Yeye ni mkarimu sana na mwenye neema, na upendo Wake haujui mipaka. Anachotaka ni watoto Wake kuwa, kumiliki, na kuishi vyema zaidi.

Sasa fikiria mstari wa leo. Ikiwa Mungu angetaka, kila mmoja wetu angekuwa katika hali ya uroboti au sanamu ambapo Mungu huvuta tu kamba, na hatungekuwa na chaguo ila kutii. Hakika ana uwezo wa kufanya hivyo; Pamoja na yote, yeye ni Mungu Mwenyezi! Badala yake, Yeye kwa upendo hutupatia uwezo wa kuchagua kwa uhuru. Mtu anaweza kuchagua kumpenda Mungu au kutompenda. Unaweza kuchagua kumtumikia Yeye au kujitumikia mwenyewe. Chaguo ni lako. Alikupa kama zawadi, kwa hiyo uwe na hekima ya kutosha kufanya chaguo sahihi.

Kumbuka Warumi 11:29, inasema , "Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake." Hii inaunga mkono moja kwa moja aya yetu ya mada ya leo. Anakupa taarifa zote unazohitaji ili kufanya uchaguzi bora zaidi na kukuambia chaguo bora zaidi la kufanya, lakini kamwe hakulazimishi kufanya hivyo.

Leo, fanya uchaguzi sahihi.

## UKIRI WA KINABII

**Kila uchaguzi ninaoufanya leo utakuwa ule ambao unalingana na mpango kamili wa Mungu kwa maisha yangu katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yoshua 24:15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 9-12



**Ezekieli 36:27**
**Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda.**

Wakristo wengi ambao nimekutana nao katika miaka yangu ya huduma wanahangaika kumpendeza Mungu. Watalia na kudai kuwa wamejaribu na hawakufanikiwa. Je, nikikuambia kwamba huna haja ya kujaribu kumpendeza tena? Kwamba uwezo wa kufanya hivyo tayari uko ndani yako na unachotakiwa kufanya ni kutembea katika mtazamo huo?

Ukitazama mstari huu kwa makini, unasema waziwazi, "nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha" Je, unaona hilo? Kwa sababu ya Roho Mtakatifu ndani yako, umefanywa kuwa mwenye haki ; tayari unapendeza Mungu kimsingi.Si lazima uende kwenye mfungo ili Yeye awe vizuri nawe; hutokea kwa asili kutoka ndani! Ukiwa na ufahamu huu, usihangaike kamwe kufanya kwa usahihi.Umezaliwa na asili mpya ya Mungu ili kuishi kwa haki.Hili ni zao la haki.Uwezo wa kufanya mambo sahihi unaweza tu kutiririka kutoka kwa roho ya haki.

Toka nje leo ukijua kuwa una asili ya Mungu ndani yako ya kuwa bora!

## UKIRI WA KINABII

**Ninatabiri siku ya kuzaa matunda ya maziwa na asali leo kwa sababu ya haki ya Mungu ndani yangu. Kila kitu ninachofanya ni kamili kwa ajili ya kuendeleza Ufalme. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 5:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 13-14



GoodNews DAILY



**Yohana 15:11**
**Hayo nimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe.**

Kuna usemi wa kawaida unaosema , "Watu walioumizwa huumiza watu." Upande wa pili wa hili pia ni kweli: watu wenye furaha huwafanya watu wafurahi! Furaha ni mapenzi kamili ya Mungu kwa maisha yako. Amekupa furaha ambayo haitegemei matukio yanayokuzunguka; furaha inayotiririka kutoka kwenye roho yako na kumgusa kila mtu karibu nawe.

Sasa angalia mstari wa leo unasema: "...na furaha yenu itimizwe." Hii ina maana kwamba kuna furaha isiyotimilifu.Inawezekana kuwa na namna hii ya furaha ndani yako lakini si sawa na vile andiko hapo juu linavyoeleza.Jambo la kusikitisha ni kwamba baadhi ya wakristo wanahuzunika kila wakati kwa sababu wao wanaendesha mambo kutoka kwenye sehemu ndogo tu ya furaha.Leo wamejawa na furaha, kesho wana mito ya machozi. Neno la Mungu limetolewa kwako ili furaha yako iwe katika kipimo timilifu wakati wote!

Wakati mambo yanapokuwa magumu, badala ya kugaagaa katika kujihurumia, tangaza, "Nakataa kuchanganyikiwa na kufadhaika! Nina furaha kamili na ushindi juu ya ushindi. Aliye mkuu zaidi anaishi ndani yangu! Furaha yake ni nguvu yangu, na ninashinda kwa utukufu katika Jina la Yesu."

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu yanaangaza furaha! Ninatabiri kwamba kila mtu ninayekutana naye leo atafurahia FURAHA TIMILIFU katika Bwana! Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 14:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 15-17

# NAFIKIRI HIVYO!



**Wafilipi 4:8**
**Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.**

Mawazo yana nguvu, na yanaunda uhalisia. Kile unachofikiria, ndicho unakuwa; ni rahisi kama hiyo. Hii ndiyo sababu Neno la Mungu linazungumza sana juu ya maisha yako ya mawazo. Mawazo hupanga mwenendo wa maisha yako. Katika mstari hapo juu, Mungu hakutuagiza tu kulinda mioyo yetu dhidi ya mawazo mabaya yasipite, lakini pia alituambia hasa aina ya mawazo ya kuruhusu.

Kuna watu ambao wamesikia kitu ambacho hakikuwa cha kweli, au cha uaminifu, au safi, au ripoti nzuri, lakini walikiweka akilini mwao hadi kikatawala maisha yao na kupelekea sonona. Wengine watashikilia kinyongo cha muda mrefu, na yote ambayo hufanya ni kuleta hali mbaya zaidi. Usiatamie mawazo juu ya kitu chochote ambacho kinaweza kuharibu roho yako. Badala yake, jizoeze kutengeneza picha zinazofaa akilini mwako kwa kupatana na Neno. Fikiria hivyo!

## UKIRI WA KINABII

**Ninafikiri tu juu ya mambo ambayo ni ya kweli, ya staha, ya haki, safi, ya kupendeza, ya ripoti nzuri ya wema na yenye sifa njema. Hatimaye nitafanikiwa, katika Jina la Yesu, haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yoshua 1:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 18-20, Zaburi 11, 59



**Warumi 12:2**
**Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.**

Umewahi kuona tabia za watu mwanzoni mwa mwaka mpya? Yote ni kuhusu kuanza upya. Wanafanya maamuzi juu ya kuhama nyumba, kubadilisha mwonekano, mavazi, kubadilisha magari , orodha haina mwisho . Yote hii inafanywa kama njia ya "kugeuza jani jipya." Kwa kubadilisha muonekano wao, wanahisi mabadiliko ya kudumu yataundwa ndani. Udanganyifu ulioje!

Biblia iko wazi linapokuja suala la mabadiliko kamili ya Mkristo. Inasema kufanywa upya nia yako, rahisi! Ulivyo leo ni zao la hali ya akili yako. Mithali 23:7 inatupa ufichuzi juu ya hili. Inasema, " maana mtu aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo..." Unaweza tu kuwa mzuri kama vile unavyojiona kuwa. Hujabadilishwa kwa sababu hatimaye ulipungua uzito na kuvaa suti bora zaidi sasa, hapana! Kubadilika kwa Mungu ni halisi. Inaanza kutoka ndani kwenda nje. Kaa katika Neno na ujitahidi kuwa mwanamageuzi halisi.

## UKIRI WA KINABII

**Ninatamka mwanzo wa mageuzi kamili katika maisha yangu. Ninapokuwa na faragha na Bwana, akili yangu itafanywa upya kila siku katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 4:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 21-24



**Wakolosai 1:12-13**
**mkimshukuru Baba, aliyetustahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru. Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake;**

Ona kwamba andiko hili liko katika wakati uliopita. Inasema kwamba Mungu alitukomboa kutoka katika nguvu za giza, si kwamba Yeye yuko karibu, au atakukomboa ukifika kanisani Jumapili - tayari imefanywa. Shetani ni adui aliyeshindwa! Anajaribu kupanda mawazo ya kujiua, mawazo ya kifo cha mapema, mawazo ya ugonjwa wa kudhoofisha, n.k. Kisha unakuta Wakristo wanakimbia kutoka kanisa hadi kanisa kutafuta "ukombozi" kutoka kwenye hofu hizi au "mashambulizi." Naam, kwa kuzingatia andiko hapo juu, usikose usingizi kwa ajili ya Shetani. Anajua kuwa ameshindwa na hana uwezo bali anawinda ujinga na woga wa watu. Wewe ni mkuu kuliko yeye, hata kama umeyatoa maisha yako kwa Kristo dakika chache zilizopita.

Bwana Yesu anasema katika Marko 16:17 "... Kwa jina langu watatoa pepo. " Anazungumza juu yako! Alikupa uwezo wa KUTOA pepo, sio nguvu ambazo ni ndogo sana kiasi kwamba shetani anapaswa kufukuzwa kwako kila wiki wakati wa ibada ya ukombozi. Usimpe shetani nafasi. Ikiwa atajaribu kujidhihirisha popote karibu nawe, ujue wewe ndiwe mwenye hatamu!

## UKIRI WA KINABII

**Ibilisi ameshindwa na atashindwa daima. Ninabeba Roho wa Mungu ndani yangu; kushindwa hakutakuwa katika msamiati wangu, kwa jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 4:4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 7, 27, 31, 34, 52



**Yohana 16:23-24**
**Tena siku ile hamtaniuliza neno lolote. Amin, amin, nawaambia, Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu.**

Mungu asingetutaka tuombe kama hangepanga kujibu maombi hayo. Alisema hasa, "... mkimwomba Baba kwa jina langu," kwa sababu alipanga kujibu. Elewa kwamba maombi ni njia yetu ya kufanya nguvu za Roho Mtakatifu kuleta mabadiliko katika ulimwengu huu. Unaweza kutarajia matokeo ya uhakika unapoomba, kaka na dada.

Mungu anafurahi kukuona ukiwa na ukizaa na kuwa na matunda. Katika maandiko ya leo, Anasema, "…Nanyi mtapata, ili furaha yenu iwe timilifu." Unaona hilo? Anataka maisha yako yawe na furaha! Watu wengine hawajui hili, kwa hiyo wanachoka kwa urahisi na kuacha kuomba kabisa ikiwa jambo moja waliloomba halikutimia . Laiti ungejua kwamba utukufu wa Mungu unaonekana katika maombi yaliyojibiwa! Thubutu kuamini, kwamba mwaka huu utakuwa mwaka wa maziwa na asali kwako NA tarajia majibu unapoomba!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana anafurahia kujibu maombi yangu. Kwa hiyo leo natangaza kwamba kila neno ninalolisema katika maombi linatimia kwa jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 3:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 56, 120, 140-142



**Waefeso 3:20**
**Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu.**

Je, unajua kwamba una uwezo wa ajabu wa Mungu ndani yako? Mtu anahitaji kutafakari swali hili kwa uzito kabla ya kuendelea. Watu wengi sana wa thamani wa Mungu wanateseka kwa sababu hawaamini kabisa jambo hili. Sikiliza, ulipompokea Roho Mtakatifu ndani yako, nguvu hizo zilianza kufanya kazi ndani yako. Zinapita kwenye mishipa yako, ziko kwenye mifupa yako, kwenye misuli yako, ziko juu yako, haleluya!

Sasa, ona hili. Katika Mathayo 10:8, Bwana Yesu alisema, "Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure.

Sasa niambie ndugu yangu, dada yangu, kama hukuwa na nguvu, kwa nini unaambiwa kufanya jambo linalohitaji nguvu za Mungu? Uliambiwa utumie nguvu kufanya mambo haya yote kwa sababu UNAYO; KWA HIYO, UNAWEZA KUTOA! Utukufu ni kwa Mungu!
Songa mbele na utumie ulichonacho leo.

## UKIRI WA KINABII

**Nguvu za Mungu zinadhihirika kupitia mimi. Nimejawa sana na nguvu hizi; Nitaponya wagonjwa, nitawatakasa wenye ukoma, nitafufua wafu, nitawatoa pepo na kufanya miujiza kwa jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Matendo 3:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 25-27



**Wagalatia 5:16**
**Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.**

Biblia inapozungumza kuhusu mwili wako, inazungumza kuhusu mambo unayotamani kufanya, hisia zako na matakwa yako. Nimeona na kusikia wengi wakilia huku wakiomba kuisulubisha miili yao. Sala hiyo si sahihi. Huhitaji kuhangaika ili mwili wako upatane na Neno la Mungu; jaza tu mawazo yako na maneno ya Kristo. Ni kutembea tu katika Roho katika ushirika wa kudumu na Mungu kunakokusaidia kuushinda mwili na tamaa zake.

Bwana Yesu anapokuwa ni Bwana wa mwili wako, unafanya kile ambacho Paulo alieleza katika Warumi 12:1, unautoa mwili wako kuwa dhabihu iliyo hai, takatifu na ya kumpendeza Mungu kwa sababu mwili wako ni mwili wake . Mwili unaoishi ndani yake ni mali ya Mungu. Unaishi ndani kama mpangaji na msimamiz; unautunza kwa ajili ya Mungu. Kwa hiyo, kuwa na nia ya Kristo; kwa kuwa hivyo, unakuwa bwana juu ya mwili wako na kufisha matendo ya mwili.

## UKIRI WA KINABII

**Akili yangu imejitoa kikamilifu kwenye Neno la Mungu ninapotembea katika Roho. Sitapambana kamwe na tamaa ya mwili kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:5

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 17, 35, 54, 63



**2 Timotheo 2:15**
**Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.**

Ili kuwa Mkristo mwenye ufanisi, ni muhimu sana kwamba ujifunze, kuelewa na kuishi kulingana na Neno la Mungu. Maandiko ya leo yanadokeza kwamba kila Mkristo lazima ajue jinsi ya kulichambua Neno na kulishiriki na wengine. Tatizo katika Kanisa tuna watu ambao hawatakosa ibada; watachukua kumbukumbu za kila kitu kinachohudumiwa, kupigia mstari maandiko na kamwe hawatajifunza kile walichosikia au kukiandika wenyewe.

Neno linapaswa kujifunza . Soma Biblia yako nyumbani na uwasomee watoto wako pia. Baadhi ya watu hufungua Biblia zao Jumapili tu kanisani. Tatizo katika hili ni kwamba unakuwa na njaa ya kiroho. Huna uwezo wa kutosha wa kukabiliana na changamoto zozote zinazokukabili, na hatimaye unakuwa Mkristo aliyechanganyikiwa. Mungu anasema katika Hosea 4: 6, " Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa. " Unaona hivyo ?

Fanya kusoma Biblia kuwa mazoea ya kila siku na utaona maisha yako yakibadilika.

## UKIRI WA KINABII

**Leo ninafanya uamuzi wa kujifunza na kujiimarisha katika Neno kuliko siku zozote. Sizuiliki na nimelishwa vyema katika maeneo yote, kwa jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 8:31

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Samweli 28-31, Zaburi 18



GoodNews DAILY



**Zaburi 82:3-4**
**Mfanyieni hukumu maskini na yatima: mtendeeni haki aliyeonewa na fukara. Mwokoeni masikini na mhitaji;**

Baraka yako si kwa ajili yako peke yako. Wakati unapozingatia tu starehe zako mwenyewe na usijali mtu mwingine yeyote, unakuwa umepotea. Misheni ya maisha ya baadhi ya watu ni kuhakikisha kodi yao ya nyumba imelipwa, watoto wao wanalishwa na shuleni, jokofu limejaa, na gari lao linaendeshwa - ndivyo hivyo! Wanaridhika tu na kukidhi mahitaji yao ya kibinafsi na kufuata ndoto zao wenyewe. Maandiko ya leo yanakuambia wewe ni zaidi ya hapo. Unaweza kubadilisha maisha ya wahitaji.

Kama nahodha wa kizazi, mtetezi wa maskini na wasio na baba, usiwahi kukunja mikono yako na kutazama shetani akiharibu mataifa na maisha ya wanadamu. Mungu anatazamia tufanye jambo fulani kwenye hili. Angalia kwa ukaribu jumuiya yako leo. Nani anahitaji ada ya masomo? Ni sera gani mbovu zinahitaji kubadilishwa katika shule au vyuo vikuu vya eneo lako? Je, kuna mzee anayehitaji upendo na matunzo yako? Una kile kinachohitajika kubadilisha mkondo wa ulimwengu wako na wengine. Unaweza kumkomboa mtu kutoka kwenye umaskini na kutetea wasio na sauti katika jamii, pia. Weka hili katika matendo unapotoka leo.

## UKIRI WA KINABII

**Utu wangu wote uko kwenye huduma ya Bwana. Nitatumia rasilimali, sauti na uwezo wangu kuwatetea wahitaji. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yeremia 22:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 121, 123-125, 128-130

GoodNews DAILY



**Zaburi 82:6**
**Mimi nimesema, Ndinyi miungu; na wana wa Aliye Juu nyote pia.**

Kuna wakati unasikia Wakristo wakisema mambo kama; "Mimi ni mwanadamu tu," au "Mimi ni mtu wa kawaida kabisa." Kwa kweli wanaamini kwa kusema kauli kama hizo mara moja wanadhihirisha unyenyekevu. Hiyo sivyo. Maongezi ya namna hii yanaonyesha ujinga wa hali ya juu kabisa.

Elewa kwamba ulikuwa wa kawaida sana hadi ulipozaliwa mara ya pili. Baada ya hayo, ukawa hazina ya nguvu, hekalu hai la Bwana Mungu Mwenyezi. Kwa kuungwa mkono na mstari wa leo, ruhusu ukweli huu kuja katika ufahamu wako. Mpaka pale utakapoifahamu, nguvu iliyomo haitafanya kazi kwako. Usiseme tena , "Mimi ni binadamu wa kawaida tu." Ulipopokea Ubwana wa Yesu Kristo, ukawa mungu. Ulizaliwa na Mungu kihalisi na mshiriki wa asili yake ya Uungu. Kumbuka Yohana 4:17 inasema, " … kama Yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwengni humu. Uko kama Baba yako haleluya!

Wakati mwingine unapojaribiwa kusema mimi ni binadamu tu, sema badala yake, "Mimi ni zaidi ya bora"

## UKIRI WA KINABII

**Nina hazina isiyokadirika, Mungu ndani yangu, anifanyaye mungu pia. Leo ninaamsha ukweli huu zaidi ya hapo awali, Kristo ndani yangu tumaini la Utukufu. Ninashindwa katika nini? SIFURI, HAKUNA KABISA, kwa jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 10:34-35

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Samweli 1-4



**Yohana 6:63**
**Roho ndiyo itiayo uzima ; mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima.**

Niliwahi kuona kichwa cha habari kilichosema, "UNAKUWA KILE UNACHOKULA." Ni kweli kile unachokula kinaathiri mwili wako, kizuri au kibaya, mwili wako unaitikia kwa namna moja au nyingine, ndivyo ilivyo kwa roho yako. Unapotumia Neno, linakuwa kitu kimoja na roho yako na kuanza kufanya kazi pale linapohitajika.

Maandiko yanazungumzia maneno ambayo ni roho, maneno yatiayo uzima. Kinyume cha hii pia ni kweli. Kuna maneno hasi ambayo pia ni roho lakini hayaleti uhai . Kama vile sio kila chakula ni nzuri kwa mwili wako, sio maneno yote ni mazuri kwa roho yako. Jitahidi kujifunza na kutafakari Neno la Mungu kuliko wakati mwingine wowote mwaka huu. Weka chini riwaya au magazeti na uweke kipaumbele kwenye Neno la uzima. Lifanye liwe mkate wako wa kila siku. Jiambie sitakula chakula kama sijakula Neno au kuomba. Linapoingia ndani yako kama Neno, basi linaishi ndani yako kama Mungu. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi nasema maneno tu ambayo Baba yangu amesema juu yangu. Maisha yangu ni maisha ya maziwa na asali ; mafanikio, ustawi, afya njema na amani, katika jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yoshua 1:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 6, 8-10, 14, 16, 19, 21



**Waefeso 3:8**
**Mimi, niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote nilipewa neema hii ya kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika.**

Ikiwa kuna andiko moja linalothibitisha kwamba Mungu hawatumii watu waliofuzu kila wakati, ni hili. Paulo aliaminiwa kufanya mengi sana katika Ufalme lakini alijitangaza kuwa yeye ndiye aliyestahili kidogo sana. Wengi wanaosoma hili wana hakika kwamba Mungu hawezi kuwatumia kamwe kwa sababu " hawakidhi " vigezo fulani. Ona kile ambacho Paulo anasema: "Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia ili awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu" ( 1 Wakorintho 1:27 ).

Mungu alikuita na kukujaliza uwezo usio wa kawaida wa kufanya kazi yake. Kwa hivyo, usijidharau au kufikiria kuwa hakuna kitu maalum kuhusu wewe. Amekufanya uwe na uwezo, si kwa sababu ya hadhi yako katika jamii au jinsi ulivyofanya vizuri chuoni; yote ni kwa neema yake. Jifunze kutazama zaidi ya uwezo wako wa kimwili. Daima kumbuka kwamba wewe ni maalum Kwake, na amekuwezesha Ki-Mungu kutimiza mgawo wako.

## UKIRI WA KINABII

**Nimetengwa kwa wakati kama huu. Nitaenda juu na zaidi ya kile nilichotarajia kufanikiwa maishani, katika jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 3:5

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Mambo ya Nyakati 1-2



**Luka 5:16**
**Akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba.**

Ninapenda jinsi Biblia inavyokuwa halisi sana hata unaweza kufuata kanuni kwa urahisi. Maandiko yanasema Bwana Yesu Kristo alijitenga na kuomba. Kwa ufupi, Alikuwa na nyakati ambapo aliacha kila kitu nyuma ili kuwa na faragha na Mungu. Wakristo wengi huomba tu wanapohisi hivyo au wakati unapowafaa wao kuomba. Kumbuka, sisi ni askari Wakristo, na askari wana nidhamu. Katika jeshi, hufanyi mambo wakati au kwa sababu unajisikia hivyo; unafanya mambo kwa sababu ni lazima uyafanye. Unashikamana na ratiba; visingizio havikubaliwi.

Tunasema sisi ni wafuasi wa Kristo. Kwa hivyo tunaiga maisha Yake ya maombi, pia. Marko 1:35 inasema, "Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka, akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko". Panga nyakati za kibinafsi za maombi kama sehemu ya utaratibu wako wa kila siku. Wakati tumepanga maombi ya pamoja kama kanisa, nyakati hizo ni muhimu pia - usizikose .

OMBA!

## UKIRI WA KINABII

**Ninatabiri maisha ya kina zaidi ya maombi kwa ajili yangu na wale wanaonizunguka . Kwa maneno ya maombi yetu, tutafanya mabadiliko katika ulimwengu wetu katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 18:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 43-45, 49, 84-85, 87



**Wakolosai 3:17**
**Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.**

Watu wengi wanaomba kwa Jina la Yesu; lakini kwa wengine, ni mazoea tu ya kidini au nenosiri. Wengine hata hawaamini wanachosema, lakini wanaomba katika Jina Lake hata hivyo na kutumaini mema. Akina kaka na dada, ikiwa tu mmeelewa kikamilifu jinsi Jina hilo lilivyo na nguvu! Lina nguvu sana kiasi kwamba linapoitwa , kila mtu hujisalimisha kwake Mbinguni, Duniani na chini ya Dunia. Hakuna na hayupo mtu anayeweza kupinga nguvu katika jina hilo na Mungu kwa neema akatupa Jina la Yesu ili tuishi kwalo. Ni neema iliyoje!

Unapoambiwa ufanye kila kitu katika Jina la Yesu, unakumbushwa kwamba una Jina la kutoa pepo, kuangamiza magonjwa, na kuleta uzima ! Hakuna kinachoweza kuingia kwenye mfumo wako au kukaa kwa sababu ya jina hili. Umepewa mamlaka mengi sana ambayo yanaweza kukufanya utawale sio tu katika maisha yako bali kushawishi na kutawala mataifa kwa Habari Njema ya Bwana wetu Yesu Kristo!
Kwa hiyo chochote unachofanya leo, fanya yote katika Jina la Bwana Yesu liwezalo! Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Kila ombi ninalofanya leo kwa Jina la Yesu linajibwa . Nitafanikiwa kama vile kinywa changu kisemavyo. Utukufu ni kwa Mungu. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 2:9-11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Mambo ya Nyakati 3-5



**Zaburi 1:3**
**Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake; wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa.**

Leo ni mwisho wa wiki nyingine ya kazi katika mwaka wa maziwa na asali. Ingawa wengine wanafurahi na kumshukuru Mungu kwa wiki yenye matokeo, wengine wanatazama nyuma kwa moyo uliojaa majuto ya majuma yaliyopotea. Mungu alikuleta katika maisha ya utele. Maisha ya kuzaa matunda, nguvu na tija. Kumbuka Yeye yu hai na ni mzima, anaishi ndani yako. Hakuna njia ambayo Yeye hufurahia uishi na kupata anguko baada ya anguko akiwa kando yako, la! Anakutakia mema tu.

Mstari hapo juu unasema utazaa matunda kila wakati - hiyo inamaanisha matokeo. Huanzishi biashara na ikafeli - kamwe . Biashara hiyo haina chaguo ila kuzalisha matunda. Inasema kila ufanyalo litafanikiwa! Toka nje leo ukijua unaweza kufanya lolote; unaweza kuwa chochote; unaweza kupata chochote; unaweza kwenda popote; unaweza kuwa vile unavyotaka kuwa.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaamuru na kutangaza kwamba maisha yangu yatakuwa maisha ya matokeo. Lolote nifanyalo halitashindwa bali litafanikiwa kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 92:12-15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 73, 77-78



**Wakolosai 2:9-10**
**Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka.**

Mtu anayesoma hii leo anahisi "kutokamilika." Huenda unajisikia hivi kwa sababu hujapata mwanamume au mwanamke bora wa kuoana nae. Labda ni kazi ya ndoto yako ambayo haujaipata bado, au ni akaunti yako ya benki ambayo inaleta hisia hizi za "kutokamilika."

Hii hapa taarifa ya habari: Mungu anapokutazama, anaona ukamilifu. Alikuambia katika mstari hapo juu kwamba wewe ni MKAMILIFU NDANI YAKE! Kila kitu unachohitaji katika maisha yako kinapatikana kwake. Biashara iko ndani Yake, amani unayoitafuta iko ndani yake – hakuna kitu kizuri unachotamani ambacho hutakipata kwake!

Ikiwa unafikiri , "Laiti mjomba wangu angeweza kunisaidia; ikiwa tu serikali ingenipa hiki au kunipa kile, ningeweza kufanikiwa maishani," unakiri kutokamilika, na hiyo ni makosa. Una uwezo katika uwezo wa Kristo. Jazwa kabisa na ufahamu huu. Jiambie hakuna uhaba katika maisha yangu. Nimekamilika!

## UKIRI WA KINABII

**Nimekamilika katika Kristo. Kila kitu ninachohitaji kiko ndani yangu. Amani ni yangu, furaha ni yangu, afya ya Ki-Mungu ni yangu kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 1:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 1 Mambo ya Nyakati 6



**1 Yohana 1:7**
**Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Kristo, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.**

Kuna baadhi ya Wakristo ambao ni wastadi wa kuhesabu dhambi. Kama mtu anayeitwa jina la ukoo pamoja na Kristo, hupaswi kamwe ufahamu wa dhambi zako. Ukifanya hivi, unakuwa na ufahamu wa kutotaka kutenda dhambi kiasi kwamba unaishia dhambini. Mstari unasema tukienenda katika nuru (Neno) kama yeye yu katika nuru, damu ya Yesu moja kwa moja hutusafisha na dhambi zote. Ikiwa, kwa mfano, umefanya jambo baya, sema tu, "Bwana, nimekosa kwa nilichofanya; NINAPOKEA msamaha katika Jina la Yesu," na ndivyo hivyo.

Mungu hakuwahi kukuambia UOMBE msamaha. Ulipookoka, ulipokea wokovu; hukuomba. Ni sawa na msamaha; unapokea msamaha; huombi kwa sababu Damu ya Yesu Kristo ilimwagika kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako. Baadhi ya Wakristo daima wanamwomba Mungu msamaha, na kwa sababu wanaomba kitu ambacho wamepewa, hawatumii imani katika maisha yao. Unapaswa kupokea msamaha kama tendo la imani yako. Umeoshwa na kusafishwa dhambi zako. Uko huru!

## UKIRI WA KINABII

**Ninakataa kuwa na ufahamu wa kidhambi. Mimi ni haki ya Mungu katika Kristo Yesu; kwa hiyo, nina ufahamu wa kihaki kuanzia leo, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 81, 88, 92-93



**Yohana 3:16**
**Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.**

Katika mstari huu kuna baadhi ya maneno mazuri sana yaliyowekwa pamoja katika maandiko! Baba yetu wa Mbinguni ni Upendo unaofanywa kuwa mtu. Ninakuambia hivi: hujipendi kama vile "Upendo" anavyokupenda! Leo, mtu anahitaji kusikia hii tu. Mungu anakupenda sana kiasi kwamba anatamani sana mafanikio yako kuliko vile inavyoweza kuwa kwako mwenyewe. Huu ni upendo ambao hauwezi kamwe kuelewa kikamilifu . Yuko tayari na anajali zaidi furaha yako, amani, na shangwe, kuliko unavyoweza kuwa kwa ajili yako mwenyewe. Anajua kila jema unalojitakia, na anakutakia wewe zaidi.

Tatizo ni wengi wamekuwa na uzoefu mbaya na upendo wa binadamu. Wameangushwa, wamekatishwa tamaa, na kusalitiwa na wale ambao hapo awali "waliwapenda". Sasa taswira ya upendo imechafuliwa katika ufahamu wao. Sivyo hivyo kwa upendo wa Mungu. Huu ni upendo katika hali yake safi kabisa. Yeye ni Upendo wenyewe! Zama katika mikono yake inayokuongoza na umruhusu akuongoze. Jinyenyekeze chini ya ukuu wa mapenzi Yake, mashauri na hekima, kwani Yeye anakutakia kheri tu. Mtumikie kwa moyo wako wote. Mwamini Yeye kwa maisha yako. Hili litakapokuwa ufahamu wako, mapambano yako yote yatakwisha.

## UKIRI WA KINABII

**Asante, Baba Mpendwa! Ninajisalimisha na kujizamisha katika upendo Wako leo! Maziwa na asali vinafurika kama matokeo yake.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 16:27

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Mambo ya Nyakati 7-10



**Yohana 16:33**
**Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki, lakini jipeni moyo ; mimi nimeushinda ulimwengu.**

Inafariji kama nini kusoma maneno kama hayo kutoka kwa Bwana wetu Yesu! Katika ulimwengu ambao umeharibika sana na umejaa magonjwa, shida za kiuchumi, majanga, vita na ubaya kila mahali, hapa hapa, katika mstari huu, tuna njia ya kutorokea! Maneno yalisemwa na Bwana Yesu Mwenyewe , na Yeye, pia, wakati wa uandishi huu, alikuwa akiishi katika ulimwengu ambao ulikuwa na giza. Hata hivyo alikuwa amejitenga na matatizo na mivuto potovu ya siku zake kwa sababu alikuwa na mawazo ya mshindi! Alifanya hivi ili kutuonyesha jinsi ya kufanya 2024, Mungu asifiwe!

Kabla ya kuondoka nyumbani, jiangalie kwenye kioo leo na ujiambie, "Mimi ni mshindi!" Hakuna kitu katika ulimwengu huu kitakachokusukuma. Kumbuka 1 Yohana 4:4 inasema, "Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Tayari umezishinda - WAKATI ULIOPITA! Hutashinda baadaye; imeshakuwa tayari! Unaye aliye mkuu zaidi anayeishi ndani yako; kwa hiyo, wewe si mwathirika. Wewe ni mshindi!
Tenda na uishi kama hivyo!

## UKIRI WA KINABII

**Hakuna hali ngumu katika ulimwengu huu litakaloniathiri. Ninaye aliye mkuu zaidi anayeishi ndani yangu, na ushindi wangu umepangwa katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 5:4-5

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 102-104

# OUR MINISTRY IS THE BIGGEST STAKEHOLDER IN THE PROPHETIC



**Prophet Uebert Angel** is the Founder of Spirit Embassy The GoodNews Church and is regarded as the godfather of the modern-day prophetic movement. He is a leading global voice and pioneer of cutting-edge prophetic demonstrations, thus being the biggest stakeholder in the prophetic, as God has called him to lead the prophetic movement in this last dispensation.

Spirit Embassy The GoodNews Church is also synonymous with deep revelations, miracles, signs, and wonders as well as unique manifestations of the power of the Holy Spirit. As the prophet to Christianity, Prophet Angel has also raised powerful men and women of God all around the world, who are making an impact in changing lives every day.



**2 Mambo ya Nyakati 29:6-11**
**Kwa maana baba zetu wameasi, na kufanya yaliyo maovu machoni pa Bwana, MUNGU wetu , na wamemwacha, na kugeuzia mbali nyuso zao makao ya BWANA , NA kumpa maungo... Wanangu , msijipurukushe sasa; kwa kuwa BWANA amewachagua ninyi msimame mbele yake, kumuhudumia, nanyi mpate kuwa watumishi wake mkafukize uvumba.**

Faida pekee ya shetani ni umri wake! Ameona kuinuka na kuanguka kwa wengi na ana maarifa mengi kuhusu uzao wa familia yako. Inaweza kuonekana kama hakuna mtu anayeoa au kuolewa katika familia yako, au biashara za kila mtu zinaonekana kushindwa. Hii ni kwa sababu mifumo ya dunia imechakachuliwa ili kukufanya uyarudie makosa ya mababu zako! Walakini, kulingana na aya ya leo, ulichaguliwa kuvunja mifumo kama hii! Unaweza kuchagua kuishi katika mapenzi kamili ya Mungu, ambayo ni maisha ya maziwa na asali!

Mungu amempa kila mtu nafasi ya kujiunga na uzao wa familia yake! Una chaguo la kuwa wa ukoo wa damu Yake, ukoo wa damu ambao shetani hana uwezo nao. Unapoendelea na siku yako, tembea katika mawazo endelevu kwamba makosa ya wale waliokuja kabla yako yataishia na wewe na kamwe hayarudiwa tena !

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mvunja mifumo! Mimi ni wa ukoo wa Mungu wa mbinguni; shetani hana nguvu kabisa juu yangu wala maisha ya familia yangu kwa Jina kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 1:12-13

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Samweli 5, 1 Mambo ya Nyakati 11-12



**Warumi 10:17**
**Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa Neno la Mungu.**

Ni katika Ukristo pekee ambapo imani imejikita katika maarifa na hekima. Hii ni kwa sababu kama Mkristo, imani inategemea maarifa unayopata kutoka kwenye Neno la Mungu! Wakati ulimwengu ukiendelea kukuza maneno na vishazi kama vile, "hatua ya imani" au "imani kipofu," hizi ni kauli ambazo huwezi kujiruhusu kutamka kama Mkristo! Imani yako kwa Mungu inapaswa kutegemea kabisa Neno Lake. Kama inavyosema katika mstari hapo juu, imani huja kwa Neno la Mungu unalokusanya.

Je, umewahi kuona jinsi watu leo wanavyokubali usaidizi wa madaktari, wauguzi, au mtu yeyote anayefanya kazi katika sekta ya afya, licha ya kutowahi kuthibitisha stakabadhi zao? Hii ni kwa sababu ulimwengu umewahimiza kuwaamini madaktari, kwa misemo kama vile, "daktari huacha maisha yake kuokoa yako," na kuwa maarufu miongoni mwa wengi. Maneno haya yanajenga imani kwako kuamini uponyaji wako unakaa hospitalini. Fikiria kwamba mtu anaweza kuweka maisha yake kwa urahisi mikononi mwa mgeni kwa sababu tu ya ujuzi ambao wamekusanya kuhusu wao. Kama Mkristo, jifunze kukua katika Neno ili uweze kuwa na imani kwamba kila kitu unachotamani kinakaa kwa Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiumbe mwenye akili! Imani yangu imejikita katika ujuzi wangu wa Neno la Mungu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 11:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 133



**Wakolosai 3:16**
**Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote ; mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.**

Katika masimulizi ya Biblia kuhusu gharika maarufu, Bwana alimwamuru Nuhu kujenga safina ili kustahimili dhoruba ya mvua iliyokuwa ikikaribia duniani kote. Ijapokuwa gharika kubwa iliyozamisha majiji yote na kusababisha vifo vingi, safina ya Nuhu iliwabeba waadilifu kwa uthabiti. Hiyo ndiyo njia ambayo Mungu alitumia kuwaokoa wale waliokuwa kwa ajili yake. Tuna kitu bora kuliko safina!

Dhoruba za mfumuko wa bei, maafa, na vurugu zinavyoongezeka katika siku hizi za mwisho, ni muhimu kupinga wasiwasi na woga. Ili kupata ushindi juu ya dhoruba, tuna Neno, haleluya! Ni muhimu kusitawisha hazina kubwa ya Neno la Mungu ndani ya roho yako. Kukuza muunganiko mzuri na Neno huhakikisha mafanikio yako mazuri, bila kujali majanga ya kimataifa. Usizamishwe na taabu za mchana; tumia tu Neno, nawe utaelea juu ya yote!

## UKIRI WA KINABII

**Ninatangaza kwamba Neno la Kristo linakaa kwa wingi ndani yangu katika hekima yote. Ninazamisha roho yangu katika Neno, nikiwa na nguvu kama safina ya Nuhu. Hali ambazo zimekuwa zikizamisha biashara, kazi, na fedha kwa wengine zitatumika kama kichocheo cha kuinuka kwangu katika Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 4:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 106-107

## UPONYAJI NI RAHISI KAMA KUPUMUA



**1 Petro 2:24**
**Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki;**

Ulimwenguni, unafundishwa kwamba maradhi, tauni na magonjwa ni kitu cha kawaida katika uzoefu wa wastani wa mwanadamu. Ingawa hali hizi zinapaswa kuwa zisizo za kawaida katika kutembea kwako na Kristo! Biblia inatufundisha kwamba mara tu ulipomkubali Yesu Kristo katika maisha yako, wakati huo huo ulikataa mambo ya kawaida! Biblia inasema kwamba mambo yote yahusuyo uzima na utauwa yamegawiwa KWAKO! Kwa hiyo, maradhi na magonjwa hayana nafasi katika maisha yako kama mtoto wa Mungu!

Kote katika Agano la Kale, tunaona utasa wa watu ukitokomezwa, watu wakifufuliwa kutoka kwa wafu, na uponyaji mwingi zaidi wa kimiujiza . Katika Agano Jipya, Roho yule yule aliyeunda miujiza hiyo anatenda kazi ndani yako! Roho yule yule aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu yu hai na anapumua ndani yako! Mara tu Roho Mtakatifu alipoingia ndani yako, ulipewa uwezo wa kuyashinda magonjwa kwa maneno yako tu. Mungu amefanya uponyaji kuwa rahisi kama kupumua; anza kutamka uponyaji katika kila eneo la maisha yako leo!

## UKIRI WA KINABII

**Ninapokea uponyaji wangu leo! Mungu amefanya uponyaji kuwa rahisi kama kupumua! Hakuna chenye uwezo wa kunidhuru au kuniangamiza, katika Jina kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 10:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Mambo ya Nyakati 13-16



**1 Yohana 2:15-17**
**Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita , pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu anadumu milele .**

Kristo anaishi, anapumua, na anafanya kazi moja kwa moja kupitia wewe! Mara tu ulipomkubali katika maisha yako, mara moja ulikubali asili yake na utamaduni wa kimungu! Kama Mkristo, unapaswa kuendelezwa upya na Neno la Mungu! Ingawa sisi sote tuna tabia za kipekee, haiba na tunayopendelea, sisi ni wafuasi wa Mungu mmoja, ambaye ni Yesu Kristo! Biblia inasema kila akaaye ndani ya Kristo anapaswa kuenenda kama jinsi Alivyoenenda!

Upotovu wa maadili wa ulimwengu ni dhahiri kwa wote kuona! Kama mtoto wa Mungu kataa kukubali tamaa na tamaduni za ulimwengu kwa kujua kwamba umechukua utamaduni wa Yesu Kristo mara tu ulipomkubali katika maisha yako! Ukiwa na utamaduni wa Kristo, unaanza kuishi msimu wa utele, baraka na utimilifu.

## UKIRI WA KINABII

**Vita ya utamaduni dhidi ya Kristo tayari imeshinda ! Nimeushinda ulimwengu na tamaa zake zote za mwili, katika Jina kuu la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 12:2

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 1-2, 15, 22-24, 47, 68



**Yakobo 5:16-17**
**... kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe, na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi sita.**

Biblia inapomtaja mtu mwenye haki, inarejelea wewe ambaye umezaliwa mara ya pili. Kwa kuzingatia hili, aya ya leo ilitolewa kwetu kama mfano wa ufanisi wa juu wa maombi katika kuchukua hatamu dhidi ya hali zetu.

Maombi ya Eliya yalikuwa ya bidii, ikimaanisha ya kutoka moyoni, yenye mwendelezo na ya juhudi. Aliomba mabadiliko, na mbingu zikaitikia.

Kwa kutawala kupitia maombi, biashara yako inaanza kutiririka kama maziwa na asali, akaunti yako ya benki, au afya yako inarejeshwa. Je, kuna lolote ungependa kulibadilisha mwaka huu? Haijalishi unapitia nini, tengeneza njia yako mbele, ukijua kwamba unaitawala na kuibadilisha kupitia maombi yako yenye ufanisi!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi katika mamlaka kamili juu ya kila kitu maishani mwangu! Hakuna kitakachoshindikana au kuanguka chini kwa sababu nimesema hivyo, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mwanzo 1:28

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 89, 96, 100-101, 105, 132



**Mwanzo 4:15**
**BWANA akamwambia, kwa sababu hiyo yeyote atakayemwua Kaini atalipizwa kisasi mara saba. BWANA akamtia Kaini alama , mtu amwonaye asije akampiga.**

Biblia inatuambia kuhusu Kaini (mzaliwa wa kwanza wa Adamu na Hawa) na ndugu yake Abeli, wakitoa dhabihu kwa Mungu. Sadaka ya Kaini, bila kujali, ilikataliwa , huku ya ndugu yake Abeli ilikubaliwa. Kwa sababu ya wivu mbaya na hasira, Kaini akamuua Abeli ndugu yake; pamoja na hayo, Mungu alimpa Kaini riziki ya juu zaidi, akimtia alama ili yeyote aliyepanga kumdhuru kwa ajili ya kosa lake apate kisasi cha Mungu mara saba!

Mara tu ulipofanyika kuwa mfuasi wa Yesu aliyezaliwa mara ya pili, ulipokea chapa hiyo hiyo ya Kristo! Bila kujali makosa au dhambi zako, umetiwa chapa ya Mungu, maana yake kila adui anayejaribu kukuweka kwenye hatari anajaribu kwa bidii kupigana na Mungu, ambayo ni vita ambayo hakika watashindwa! Hisia hii iliungwa mkono na Mtume Paulo aliposema, “Tangu sasa mtu awaye yote asinitaabishe; kwa maana ninabeba chapa za Bwana Yesu.” Kuanzia leo na kuendelea, hakuna mtu atakayekusumbua kwa sababu umewekwa chapa na Kristo !

## UKIRI WA KINABII

**Ninabeba chapa ya Kristo! Adui yeyote anayejaribu kuniangamiza atapata kisasi cha Mungu mara saba! Hakika HAKUNA anayeweza kunishinda! Kwa hakika kama jua linapochomoza asubuhi, sitashindwa kamwe katika Jina kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wagalatia 6:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 2 Samweli 6-7, 1 Mambo ya Nyakati 17



**Mwanzo 2:18-22**
**BWANA Mungu akasema si vema huyo mtu awe peke yake... BWANA Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake; Na ule ubavu alioutwaa katika Adamu BWANA Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu.**

Mara nyingi, unaweza kung'ang'ana bila msaada kutafuta masuluhisho ya masuala mbalimbali unayokabiliana nayo katika maisha yako ya kila siku bila kutambua kikamilifu kwamba kila kitu unachohitaji kiko ndani yako! Biblia inatuambia kwamba Adamu (mtu wa kwanza) alipata upweke bila kutambua tiba ya upweke wake ilikuwa inakaa ndani yake!

Mungu amekupa mamlaka juu ya hali zote za maisha yako! Kama mtoto wa Mungu, umeketi pamoja na Bwana Yesu katika ulimwengu wa roho. Kujiruhusu kushindwa au kuishi maisha chini ya hali ya wastani ni kupinga utambulisho wako katika Kristo! Je, umegundua wewe ni nani hasa katika Kristo? Wewe ni mtu wa mafanikio; wewe ni utukufu wa Mungu; una nguvu ya uponyaji ambayo inaweza kutoa afya katika kila nyuzi za utu wako! WEWE NDIYE SULUHISHO!

## UKIRI WA KINABII

**NAJUA MIMI NI NANI NDANI YA KRISTO! Mimi ndiye suluhisho! Mungu amenifanya kuwa ufunguo wa kufungua mlango wowote uliofungwa. Katika mwaka huu, nitamshtua kila mtu aliyenitilia shaka, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
**2 Petro 1:3-4**

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 25, 29, 33, 36, 39



**Warumi 12:1**
**Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.**

Mara tu unapozaliwa mara ya pili, ni kazi yako kuutunza mwili wako, ambao ni hekalu la Mungu. Ni juu yako kutunza afya na nguvu ili Mungu akutumie. Shetani atajaribu kuudhuru mwili wako, lakini una uwezo wa kusema hapana na kumzuia.

Kumbuka kile mstari wetu mkuu unasema: "Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai." Mungu anakupa mamlaka ya kuusimamia mwili wako. Ndio maana baadhi ya wakristo, ingawa wana Roho Mtakatifu, bado wanapambana na magonjwa. Ni kwa sababu wao ndio wanaosimamia miili yao. Mungu anayo haki ya kutawala mwili wako, lakini alikuteua uutunze kwa ajili yake. Kwa hiyo leo, inuka kupitia Neno na utawale nyumba yako, ambayo ni mwili wako. WEWE NDIYE MWENYE HATAMU, na kila kitu ni kwa faida yako!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ndiye mwenye hatamu; ugonjwa sio sehemu ya mimi. Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo, na amefanya njia kwa ajili ya afya yangu ya Ki-Ungu. Ninakataa kuwa mgonjwa! Ninaishi maisha ya maziwa na asali na Mungu anayeniweka katika afya njema. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 6:19-20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 2 Samweli 8-9, 1 Mambo ya Nyakati 18



**Mithali 24:16**
**Kwa maana mwenye haki huanguka mara saba akaondoka tena; Bali wasio haki hukwazwa na mabaya .**

Ustahimilivu ni moja ya kanuni muhimu kwa wale wanaotaka kupata maisha ya mafanikio! Biblia inatuambia kisa cha kijana mdogo anayeitwa Yusufu ambaye alikuwa na uwezo wa kufasiri ndoto. Ndugu zake Yusufu walimwonea wivu na kumuuza utumwani Misri. Miongoni mwa changamoto nyingi alizokabiliana nazo alipokuwa Misri, ni kusingiziwa kwa uwongo , jambo ambalo lilipelekea kufungwa kwake. Hata hivyo, uwezo wake wa kufafanua ndoto ulimfikia Farao, na hivyo kumfanya apate mamlaka akiwa mshauri mwenye kutegemewa na wa pili katika uongozi katika taifa zima!

Yusufu ni mmoja tu wa watu wengi katika Biblia ambao walionyesha umuhimu na nguvu ya ustahimilivu. Bila kujali hali za maisha, kumbuka kwamba mambo yote hufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wanaompenda Mungu! Unapoendelea kwa muda wote wa juma lako, thibitisha mara kwa mara Ubwana wa Yesu Kristo juu ya kila hali kuhusu maisha yako na maisha ya familia yako. Utauona mkono wenye nguvu wa Mungu ukifanya maajabu katika maisha yako!

## UKIRI WA KINABII

**NINAISHI MAISHA YA USTAHIMILIVU BILA KUJALI CHANGAMOTO, nitashinda na kuzidi matarajio ya kila mtu. Katika mwaka huu, MACHO YANGU YATASHUHUDIA WEMA WA MUNGU! Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 28:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 50, 53, 60, 75



**Danieli 12:3**
**Na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga, na hao waongozao wengi kutenda haki kama nyota milele na milele.**

Hakuna furaha kubwa kuliko kumpendeza Bwana na kutimiza mapenzi yake kwa kuwaongoza wenye dhambi kwenye wokovu. Huwezi kudai kuwa Mkristo makini bila kutanguliza wito wako wa kuhudumu Injili kwa wengine.

Bwana Yesu Kristo Mwenyewe alitoa muhtasari wa utume Wake hapa Duniani aliposema, "Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea" ( Luka 19:10 ) . Unaona hilo? Ikiwa tunadai kuwa kama Kristo, basi utume Wake unapaswa kuwa utume wetu.

Kama Wakristo, tumeitwa kutimiza huduma ya upatanisho na kujihusisha kikamilifu katika kuvuna nafsi kama mtindo wa maisha, si tu jambo tunalofanya mitaani kama kikundi cha kanisa mwishoni mwa juma. Maziwa na asali huashiria utele, baraka na utimilifu. Shiriki hilo na mtu leo!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mmishonari aliyetumwa kwa wakati kama huu! Leo nitatumia kila nafasi kumsaidia mtu kupokea zawadi ya thamani ya wokovu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 28:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Samweli 10, 1 Mambo ya Nyakati 19, Zaburi 20



**1 Yohana 5:4**
**Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu, na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.**

Wakristo wengi mara nyingi hutaja mstari hapo juu bila kufahamu kikamilifu maana ya kuushinda ulimwengu. Ukiisha kuushinda ulimwengu, unakuwa na uwezo na mamlaka ya kutiisha mifumo ya kidunia. Neno 'kutiisha' maana yake ni kuleta kitu chini ya himaya au udhibiti wako! Hivi ndivyo Biblia inavyosema tumeufanyia ulimwengu na mifumo yake!

Kama mtoto wa Mungu, wewe ni mrithi pamoja na Kristo! Biblia inatuambia kwamba mambo yaliyopo na yajayo ni yako! Kila mara, thibitisha wewe ni nani katika Kristo, ukisema, "Mimi nina mamlaka juu ya vitu vyote; ulimwengu ni wangu!" Una hati ya kisheria juu ya hilo - Neno la Mungu! Kwa hivyo, haijalishi ni nini kinachotokea karibu nawe, bado una uwezo wa kutiisha mifumo ya ulimwengu kwa faida yako!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni wa Mungu na nimeushinda ulimwengu! Mimi ni Mungu-mtu, ambaye Kristo anakaa ndani yake kihalisi. Mungu amenipa mamlaka juu ya mambo yote yanayohusu uzima na utauwa. Sipungukiwi chochote; utajiri wangu hauna kikomo, haukadiriki, na hauwezi kupimwa . Nimeshinda kila uwezo na nguvu zinazojaribu kuinuka dhidi yangu, katika Jina kuu la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 3:21-22

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 65-67, 69-70



**3Yohana 1:2**
**Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo .**

Mpango wa ajabu wa Mungu kwako ni mafanikio kamili. Anataka ustawi kwa kila njia - katika roho yako, katika afya yako, na katika fedha zako. Unaweza kuwa unafanya vyema katika imani yako katika eneo moja lakini bado unapambana na magonjwa au matatizo ya pesa. Lakini Mungu anataka uwe nayo yote pamoja - kiroho, kimwili, na kivitu. Hilo ndilo lengo la Mungu - aina ya ustawi wa uwiano ambapo kila nyanja inastawi.

Mstari huo pia unazungumza juu ya ustawi wa kiroho kuwa kipaumbele. Mungu anataka ufanikiwe kifedha na kimwili, na pia anataka uwe na afya njema. Ukiwa na afya njema, huhitaji uponyaji kwa sababu hauugui. Ni ajabu, sio? Lifanye litendeke kwa kuliishi Neno! Jizamishe ndani yake, jifundishe, lifikirie, na litakuwa nuru inayoongoza kwenye mafanikio kamili!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtu wa Neno, na ninaamuru na kutangaza kwamba nina mafanikio kamili kupitia Neno leo katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 4:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 2 Samweli 11-12, 1 Mambo ya Nyakati 20



**Warumi 1:16**
**Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye; kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia .**

Ni Habari Njema ya Bwana wetu Yesu Kristo pekee inayoweza kumweka mwenye dhambi katika nafasi ya wokovu mtukufu na haki. Hakuna njia nyingine! Ni kupitia tu kuwaambia watu kuhusu Injili ndipo Haki ya Mungu inaweza kufunuliwa na kukumbatiwa. Kinyume na uwongo wa kawaida kuhusu njia mbalimbali za kumfikia Mungu, hakuna mbinu nyingine za kumpata Kristo isipokuwa mtu anahudumiwa na wokovu kukubaliwa.

Hapa ndipo unapoingia. Ikiwa bado unajaribu kubaini kile unachoitwa kufanya, hapa kuna wito wa lazima. Umepokea agizo la kupeleka Injili hadi miisho ya Dunia. Ni wito si kwa viongozi wa kanisa pekee; ni jambo unalopaswa kufanya kwa ujasiri wote, imani, umahiri, na usadikisho. Hupaswi kamwe kuona haya au kuomba msamaha kuhusu Kristo na ujumbe wa Injili. Usijionee haya wewe ni nani ndani Yake, na usiruhusu wengine wakufanye uone aibu kwa kile unachoamini.

## UKIRI WA KINABII

**Siionei haya Injili ya Kristo! Huu ni wito wangu wa juu, na ninatembea ndani yake kwa moyo wote na kwa ujasiri! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Danieli 12:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 32, 51, 86, 122

# GOODNEWS NATION EXHIBITION 2023

WITH PROPHETS
**UEBERT** & **BEBE ANGEL**

The annual GoodNews Nation Exhibition features all of the exploits and achievements of the GoodNews World Ministry including the well renowned GoodNews Daily Devotional which has made a huge impact across the world. The event takes place during the Annual Exodus Crossover Season with The Commander-in-Chief of The GoodNews World, Prophet Uebert Angel.

The GoodNews Nation Exhibition helps expand the vision and inspires faith for the future of our leaders and our partners.



The Lord has called us to fulfill a very definite purpose, which is to take His divine presence to the peoples and nations of the world, through the vehicle that is The GoodNews Daily Devotional and to demonstrate the character of His Spirit everywhere.














**Zaburi 105:1**
**...Mshukuruni Bwana ; liitieni jina lake, wajulisheni watu matendo yake.**

Kuna nguvu ya mageuzi katika ushuhuda wako! Ni jukumu lako pekee kushuhudia wema wa Mungu katika maisha yako! Mstari huo hapo juu unatuambia kwamba ni lazima tulitangaze Jina la Mungu na kuwajulisha mataifa kile ambacho ametufanyia. Kwa maneno mengine, NENDA UKAMWAMBIE MTU FULANI! Sio kila nguvu ya giza inakujua wewe ni nani au nani anakaa ndani yako. Kwa hiyo, jambo la kwanza unapaswa kufanya unapoingia eneo jipya ni kushuhudia. Unaposhuhudia, unatuma ishara katika ulimwengu wa roho ambazo hujulisha kila kiumbe kuwa wewe ni mtoto wa Mungu na nguvu zake zinatenda kazi ndani yako!

Kupitia ushuhuda wako wa kimageuzi, unawatia moyo wengine, ukiimarisha imani yao ili kupokea muujiza wao wenyewe! Biblia inatuambia kwamba kwa nguvu ya shuhuda zetu, tumeshinda mambo yote yanayojaribu kuinuka dhidi yetu. Kwa hivyo kumbuka, kaulimbiu ya mwaka ni maziwa na asali, hiyo inamaanisha kuwa shuhuda zinapaswa kuwa mkate wako wa kila siku mwaka huu! Utaendelea kushuhudia kwa Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Nitashuhudia popote niendapo na kuwaambia mataifa yote Mungu amenitendea. Ninabadilisha maisha yangu kupitia nguvu ya ushuhuda wangu! Ninaposhuhudia, mapepo yanapagawa na hofu. Katika mwaka huu, nitashuhudia zaidi kuliko hapo awali! Mawakala wa giza, kuweni makini!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Ufunuo 12:11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Samweli 13-15



**Mathayo 5:14**
**Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji ulio juu ya mlima hauwezi kusitirika .**

Wewe ni nuru ya ulimwengu! Nuru hutoa mwelekeo; kama vile nuru, wajibu wako kama Mkristo ni kutoa mwelekeo kwa wale walio katika ulimwengu jinsi maisha yanavyopaswa kuishi! Wewe ndiye wa kuwaonyesha jinsi ya kufanikiwa na jinsi ya kuwa nuru bila kujali giza. Kristo tayari alitekeleza sehemu yake kwa kupata wokovu kwa wanadamu wote kupitia kifo chake kwa niaba yetu na ufufuo wa utukufu! Sasa, ni wajibu wako kuishi maisha marefu na kuwaambia kila taifa juu ya uwezo Wake wa kuokoa!

Kama nuru ing'aayo, unaondoa giza popote unapoenda, ikimaanisha uhaba, ugonjwa, na jambo lolote baya halina nafasi katika maisha yako au ya familia yako! Acha moto wa Injili uwake daima ndani yako na kupitia kwako! Wewe ni mwakilishi wa Mungu mwenyewe hapa Duniani! Kuwa mfano kupitia kauli zako na jinsi unavyojiendesha. Wewe ndiye nuru na tumaini la ulimwengu huu, nuru ambayo haiwezi kufichwa! Thibitisha maziwa na asali ni uhalisia wako haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi maisha ya kung'aa! Nuru yangu huondoa giza. Mimi ni kama mnara wa nuru unaoleta mwelekeo kwa mabaharia waliopotea! Mimi ni mwakilishi wa Mungu Duniani! Nuru yangu itawaka zaidi kuliko hapo awali mwaka huu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 8:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 3-4, 12-13, 28, 55



**Mithali 23:18**
**Maana bila shaka iko thawabu; na tumaini lako halitabatilika.**

Katika mambo ya kiroho, tunasema imani ni mama wa miujiza, na matarajio ni mkunga. Kwa maneno mengine, ili muujiza wako uweze kujifungua salama na kwa uhakika, unahitaji mkunga mbaye ni matarajio kukusaidia kufanya hivyo!

Unaona, unapotarajia mambo ya Kimbingu, unaongeza Uungu kwenye asili yako. Haijalishi ikiwa maisha yako ni makavu . Haijalishi kama umefukuzwa kazi. Kwa kutarajia, yule asiye na kitu mkononi mwake ndiye yuleyule ambaye Mungu anamtumia kubadilisha si maisha yake tu bali wale wanaomzunguka kwa manufaa yao pia. Zikumbatie ahadi za Mungu popote uendapo na tarajia maziwa na asali kutiririka leo!

## UKIRI WA KINABII

**Ninapoianza siku yangu ya leo, nina matarajio makubwa kwamba mambo makubwa yatatokea. Muujiza wangu hauko tena karibu; umeshafika tayari! Ninarudi nyumbani na ushuhuda! Utukufu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 1:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Samweli 16-18



**1 Wakorintho 2:12**
**Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu; makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu.**

Kuishi ukawaida ni tusi kwa maisha ambayo Mungu anataka uwe nayo! Kama mtoto wa Mungu, unaishi mbali sana na mifumo ya ulimwengu huu; kwa hiyo, matendo yako lazima yalingane na kile ambacho Mungu amekuitia kuwa! Kataa mambo ya ukawaida katika maisha yako, iwe ni fedha za kawaida, furaha ya kawaida au afya ya kawaida. Biblia inasema kwamba vitu vyote vimetolewa bure kwako! Nia yake ni wewe kuishi juu ya misukosuko ya ulimwengu huu wa muda na kuishi maisha bora, maisha ya AJABU!

Hakuna kitu unachohitaji ambacho Mungu hajakupa wewe kama Mkristo. Kupitia kukua katika Neno, unajifunza yote ambayo Mungu amekupa. Unapotembea katika ufahamu wa urithi wako kama Mkristo, hakutakuwa na nafasi kwa maisha ya kawaida kuchukua katika maisha yako! Fanya upako wa Roho Mtakatifu kuwa makao yako kila siku, kua katika Neno la Mungu uone maisha yako yakitoka ukawaida hadi kuwa ya ajabu!

## UKIRI WA KINABII

**NIKATAA MAISHA YA UKAWAIDA. Mimi ni kiumbe kisicho cha kawaida; kwa hiyo, ninaishi maisha ya ubora, yanayofurika maziwa na asali. Nimezaliwa na Mungu na ninaishi kulingana na asili yake ya Uungu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 3:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 26, 40, 58, 61-62, 64



**Wagalatia 4:1**
**Lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote.**

Kuna ukweli fulani katika Neno ambao unaweza kukupita kwa urahisi ikiwa hutaenenda katika uhalisi wa DNA ya kifalme ndani yako! Ahadi ya Mungu kwa watu wake kuishi katika maziwa na asali inasimama leo kama ilivyokuwa wakati huo, lakini lazima uchague kutembea katika ukweli huo. Kulingana na mstari wa leo, ni juu yako kama Mkristo kufanya uchaguzi: je, utakuwa mrithi au mtumwa? Ukibaki katika hali ambayo hujui wewe ni nani, ambapo hukui wala hautembei katika ahadi za Mungu zinazohusu maisha yako, utakuwa mtoto na kuishi maisha ya utumwa.

Unapoishi maisha ya mrithi, haukosi chochote kwa sababu ukosefu sio urithi wako kama mtoto wa Mungu! Fanya uamuzi wa kukua kutoka utoto hadi mwana, na ufurahie kila ahadi ambayo tayari ni yako kwa haki!

## UKIRI WA KINABII

**DNA ya Mungu iko ndani yangu; kwa hivyo, sitaishi maisha ya mtumwa. Utajiri ni wangu, haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 32:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Samweli 19-21



**Wafilipi 4:6-7**
**Msijisumbe kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.**

Mara nyingi, unapitia magumu maishani mwako na hujui jinsi ya kuyatatua kwa sababu tu hukujivika na maombi yenye uwezo mkubwa! Mungu hakutuambia tuombe kwa ajili ya kuomba tu bali kwa sababu kuna nguvu maalum inayoambatana na kuomba! Kuishi maisha kama Mkristo bila maombi ni kama kutembea kwenye uwanja wa vita bila silaha! Unapoomba, unajitayarisha kwa lolote ambalo adui anaweza kujaribu kukurushia!

Mstari huo hapo juu unatuambia kwamba unaposhukuru na kuomba, wasiwasi unakuwa jambo la zamani , na amani ya Mungu ipitayo akili zote itaulinda moyo wako bila kujali hali unazokabiliana nazo. Tumia fursa ya nguvu kuu katika maombi leo!

## UKIRI WA KINABII

**Ninapoomba mambo yanabadilika! Ninajitayarisha kwa hali yoyote kupitia nguvu ya maombi yangu! Kutokana na maombi yangu, amani ya Bwana imeyameza maisha yangu, katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 18:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 5, 38, 41-42



**Mhubiri 9:11**
**Nikarudi, na kuona chini ya jua, ya kwamba si wenye mbio washindao katika michezo, wala si walio hodari washindao vitani, wala si wenye hekima wapatao chakula, wala si watu wa ufahamu wapatao mali, wala wenye ustadi wapatao upendeleo; lakini wakati na bahati huwapata wote.**

Wakristo wengi hufanya makosa kulinganisha safari yao na safari za wengine! Maneno kama, "Ninajua mahali ninapopaswa kuwa sasa," hata kama ni maarufu, si ya Ki-Mungu! Aya ya leo inatufahamisha kuwa si wenye mbio washindao. Kwa sababu haupo mahali ulipofikiri ungekuwa sasa haimaanishi kwamba Mungu amekusahau au wewe si wa muhimu sana machoni pake. Wakati wako na bahati zitakuja!

Katika duru za riadha, wanariadha wa mbio za Olimpiki wanahimizwa kuzingatia mstari wa kumalizia na kutotazama nyuma juu ya mabega yao wakati wa mbio, kwani inaweza kuwapunguzia kasi. Vivyo hivyo, unapotazama mbio za wengine badala ya kukazia fikira na njia yako mwenyewe, unaweza kupoteza mwelekeo wa mstari wa kumalizia na kujipunguzia mwendo! Jifunze kuzingatia tu kile ambacho Mungu amekuitia kuwa. Ukue katika Neno Lake kila siku, na usiwe na wasiwasi juu ya kile ambacho wengine wanafanya!

## UKIRI WA KINABII

**Niko kwenye njia yangu mwenyewe! Ninazingatia mstari wangu wa kumaliza; Siangalii begani mwangu wakati wa mbio na tayari nimeshinda kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 26:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Samweli 22-23, Zaburi 57



**Luka 5:16**
**Lakini yeye alikuwa, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba.**

Katika ulimwengu ulio na vitu vingi vya kukengeusha fikira, ni rahisi kupuuza kuwa peke yako na Mungu. Ikiwa hutambui umuhimu wa kujitenga kwa faragha, kuna mengi unaweza kukosa maishani! Ni muhimu kwa kila Mkristo kuanzisha muda wa faragha na Bwana. Kabla ya ufunuo, kuna kujitenga! Unapojifunza thamani ya kuwa na wakati wa faragha na Bwana, utastaajabishwa na matokeo ya kudumu ambayo utakuwa nayo kwenye maisha yako.

Mara kadhaa katika Biblia, tunaona Bwana Yesu alitenga nyakati za kuwa peke yake kabisa na Baba! Kila Mkristo anapaswa kujitahidi kuwa na muda kuwa ana kwa ana na Mfalme wa wafalme! Tunaishi mwaka uliotabiriwa, mwaka wa maziwa na asali. Hiyo inamaanisha utele na baraka juu ya baraka! Ziamshe baraka hizo kwa kutumia muda bora peke yako na Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Ninapokaa na Bwana peke yangu, ukubwa wa utukufu Wake katika maisha yangu unaongezeka. Nimegeuzwa sura kutoka utukufu hadi utukufu, katika Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 14:23

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 95, 97-99



**Warumi 8:5-6**
**Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili ; bali wale waifuatao Roho huyafikiri mambo ya Roho. Kwa kuwa na nia ya mwili ni mauti ; bali kuwa na nia ya roho ni uzima na amani.**

Dhana potofu iliyozoeleka miongoni mwa Jumuiya ya Wakristo ni kwamba kuyatoa maisha yako kwa Kristo ni ukamilifu wa kutembea kwako na Mungu. Hata hivyo, kuyatoa maisha yako kwa Kristo ni hatua ya kwanza katika safari yako yenye mambo mengi. Lazima uwe na ufahamu wa umoja wako na Roho Mtakatifu. Mungu amekuumba, na Mungu ni Roho, ikimaanisha asili yako kama mtoto wa Mungu ni ya Roho! Ili kuishi maisha ipasavyo, lazima uukatae mwili kila wakati! Kila unaposukumwa au kuhamasishwa kufanya jambo fulani, jiulize iwapo msukumo huo unatoka kwa Mungu, kwenye mwili wako au hata kwa Shetani!

Mrejee Roho Mtakatifu kuhusu elimu yako, kazi yako, ndoa yako na watoto wako! Unapomruhusu Roho Mtakatifu akuongoze, utapata amani inayozidi kile ambacho ulimwengu hutoa. Kufanikiwa kwako maishani kunategemea uwezo wako wa kupambanua mambo ya Roho. Hakikisha unasoma neno kila siku, ukijitenga na wale walioko duniani, na ujione kuwa nyumba yenye nguvu ya kiroho!

## UKIRI WA KINABII

**MIMI NI NYUMBA YA NGUVU ZA KIROHO! Ninaishi maisha yanayotawaliwa na Roho ya Mungu, na mwili hauna nguvu juu ya kufanya maamuzi yangu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 2:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 2 Samweli 24, 1 Mambo ya Nyakati 21-22, Zaburi 30.



**Luka 6:12-13**
**Ikwa siku zile aliondoka akaenda milimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu. Hata kulipokuwa mchana, aliwaita wanafunzi wake kwake, akachagua kumi na wawili miongoni mwao, ambao aliwaita mitume.**

Ikiwa unataka kuishi maisha ya mafanikio, ni nani unayechagua kuzungukwa naye ni muhimu! Mstari wa leo unatuonyesha jinsi Bwana Yesu alivyojua umuhimu wa aliozungukwa nao na matokeo ya kudumu ya uchaguzi huo. Anaonyeshwa akienda katika eneo la faragha na kutumia thamani ya usiku wa maombi kwa ajili ya uamuzi huu. Mara nyingi, Wakristo huchagua washirika wao kulingana na viwango ambavyo ulimwengu umeweka badala ya utambuzi wa kiroho! Usichague marafiki kulingana na iwapo mtu anafurahia vipindi vya televisheni kama wewe. Chagua watu wanaoendana na wito wako wa kiroho.

Danieli ni mfano kamili kutoka katika Biblia; alikuwa na marafiki wakubwa. Mfalme alipotoa amri ambayo ingemdhuru na kumweka katika matatizo, Danieli aliwaita marafiki zake ili waombe, na Mungu akawapa suluhisho kwa tatizo lao. Hawa ndio aina ya marafiki unaopaswa kuwa nao, marafiki wanaokuleta karibu na Mungu na kukutia moyo katika mambo yaliyo sawa!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaongozwa na Roho Mtakatifu ninapochagua ni nani ninayezungukwa naye. Ninachagua marafiki wanaonitia moyo kwenye matendo mema na kamwe si kinyume chake, katika Jina la Yesu !**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 13:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 108-110



**2 Wakorintho 4:18**
**Tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana, kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini visivyoonekana ni vya milele.**

Ingawa kwa macho ya kawaida inaweza kuonekana kama kuna mamia ya vikwazo na changamoto zinazokuzuia kutimiza malengo yako, mstari hapo juu unasema vitu vinavyoonekana ni vya muda tu! Kila "ukuta" unaoweza kukutana nao ni kikwazo tu cha kufikiria! Kama Mkristo, hakuna chochote kitakachoweza kukuzuia! Biblia inasema aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia, maana yake hakuna changamoto kabisa utakayowahi kukutana nayo ambayo ni kuu kuliko Mungu anayeishi na kutenda kazi kupitia wewe!

Katika Biblia, tunaona wanafunzi wakieneza Habari Njema ya neema ya Mungu wakati ambapo watu walikuwa na chuki sana dhidi ya Wakristo hata walifikia kuwatesa na kuwaua. Lakini kwa sababu ya michango ya wanafunzi kwa Ufalme, Ukristo unaendelea kukua miaka 2500+ baadaye. Hii ikoje? Ni kwa sababu walikataa kuona vikwazo vilivyo mbele yao! Kataa kuzingatia kizuizi chochote ambacho kimesimama kwenye njia yako ya maisha ya maziwa na asali!

## UKIRI WA KINABII

**Kabisa HAKUNA kitakachoweza kuniangamiza! Ninakataa kuzingatia kizuizi chochote ambacho shetani anajaribu kuweka katika njia yangu! KAMWE SIWEZI KUSHINDWA! Utukufu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 4:4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Mambo ya Nyakati 23-25



**1 Wafalme 18:43-44**
**Akamwambia mtumishi wake, Kwea sasa, utazame upande wa bahari. Akakwea, akatazama, na kusema, Hakuna kitu. Naye akanena, Enenda tena mara saba. Ikawa mara ya saba, akasema, Tazama, wingu dogo linatoka katika bahari, nalo ni dogo kama mkono wa mtu. Akanena, Enenda, ukamwambie Ahabu, Tandika, ushuke, mvua isikuzuie.**

Nchi ya Israeli iliteseka kwa miaka mingi ya ukame na njaa hadi Nabii Eliya alipotangaza, "Nasikia sauti ya mvua nyingi." Katika ulimwengu wa asili, sauti ya mvua haikusikika, lakini katika ulimwengu wa kiroho, Eliya aliweza kusikia sauti kuu ya mvua ikijiandaa kunyesha! Licha ya tamko la nabii, mvua haikuanza mara moja. Mtumishi wa Eliya alienda kuangalia mara sita kabla ya kuona wingu dogo lililotangulia mvua!

Wengi hufanya makosa kutafuta mvua mara moja! Usikose kamwe kuona vidokezo vidogo ambavyo Mungu anakupa ili kukuarifu juu ya wingi ujao! Jifunze kukiri jinsi Mungu amekufikisha katika maisha yako. Kwa mtazamo wa kwanza, kazi hiyo au fursa inaweza kuonekana ndogo au duni; hata hivyo, inaweza kuwa manati yako na wingu dogo kudokeza mambo makubwa yajayo! Hakikisha unaendelea. Angalia ishara za maziwa na asali! Endelea kutafuta alama za imani yako, na wingi utafuata!

## UKIRI WA KINABII

**Najua Mungu ananitayarisha kwa makubwa zaidi katika maisha haya! Katika mwaka huu, ninatambua kila wingu mbele yangu, katika Jina kuu la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yeremia 29:11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 131, 138-139, 143-145



**Mathayo 28:19-20**
**Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote. , hata ukamilifu wa dahari.**

Ulifanywa kuwa mkufunzi wa MATAIFA! Ni wajibu wako kama mtoto wa Mungu kutekeleza ushindi wa Kristo katika mji wako kwa kutangaza Ubwana wa Yesu popote unapoenda! Agizo la kuvuna nafsi limetolewa kwa kila Mkristo bila kujali umri, kazi au hata makosa. Katika Biblia, tunaona Paulo, ambaye aliwatesa Wakristo kabla ya kukabidhi maisha yake kwa Kristo, akiwa na wamisionari duniani kote ambao walisababisha zaidi ya mataifa saba kuwa mataifa ya Kikristo.

Biblia inatuambia tuhubiri kwa kila kiumbe, ikimaanisha kuna sababu za kuvuna nafsi bila kujali uko wapi duniani! Iwe shuleni, kazini, au hata kwenye mgahawa, kila mahali unapoenda ni eneo linalofaa zaidi kuvuna nafsi! Mungu yu pamoja nawe siku zote, basi usiogope kukataliwa na mtu yeyote. Uliumbwa kufanya hivi!

## UKIRI WA KINABII

**Ninachukua jukumu la kuvuna nafsi katika kazi yangu, shule na jiji! Mataifa yatajua Jina la Bwana Yesu Kristo kwa sababu YANGU! Katika mwaka huu, watu watanitaja kama MVUNAJI NAMBA MOJA WA NAFSI!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 1:15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Mambo ya Nyakati 26-29, Zaburi 127



**Zaburi 1:3**
**Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake; wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa.**

Kuna baadhi ya Wakristo wanasema, "Tusitegemee mema kila wakati kutoka kwa Mungu; wakati mwingine tunapaswa kutarajia mabaya kwa sababu maisha yamejaa kupanda na kushuka." Hiyo ni dhana mbaya sana ya ujumbe wa Injili. Mungu si mpangaji wa uovu na mateso duniani. Ndoto yake, ambayo tayari imetimizwa kwako katika Kristo Yesu, ni wewe kutembea katika mafanikio kamili. Hiyo ni pamoja na pesa lakini huenda zaidi hilo!

Unaona, hakuna mtu aliyezaliwa katika ulimwengu huu aliyekusudiwa na Mungu kuwa maskini, mgonjwa, aliyevunjika moyo, mwenye sonona, mwenye huzuni au kuteseka. Badala yake, mapenzi ya Mungu ni watu wote kufanikiwa na kuwa na afya, kama vile roho zao zinavyofanikiwa ( 3 Yohana 1:2 ). Anatafuta ustawi wa roho yako, nafsi yako, na mwili wako wa nyama. Hii ndiyo sababu hupaswi kuridhia au kukubali magonjwa, umaskini, kushindwa, au kutarajia pesa pekee; Mapenzi yake ni zaidi ya pesa. Unabii wa maziwa na asali unamaanisha kuwa kila eneo la maisha yako limefunikwa na kuzaa matunda kabisa, sifa kwa Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi maisha juu ya hali, juu zaidi hali zote. Ustawi wangu umehakikishwa na unajumuisha pesa na vitu zaidi yake. Mimi ni tajiri, katika Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 4:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 111-118



**Kumbukumbu la Torati 29:5**
**Nami miaka arobaini nimewaongoza jangwani; nguo zenu hazikuchakaa juu yenu, wala kiatu chako hakukuchakaa katika mguu wako.**

Mungu humpa kila mmoja wa watoto wake riziki bora! Biblia inatuambia kwamba Waisraeli walipowekwa huru kutoka katika utumwa huko Misri na walipokuwa nyikani, Mungu alishughulikia kila mahitaji yao. Licha ya hali ya kutisha na ukame wa jangwani, hawakuunguzwa na jua kali , nguo zao hazikuchakaa, na miguu yao haikuvimba kwa maumivu. Waisraeli walikuwa viumbe wa Agano la Kale. Nini zaidi wewe, ambaye una Roho Mtakatifu! Mungu huyohuyo anakuruzuku na kukulea leo!

Wengine hufanya makosa ya kujaribu kukabiliana na changamoto za maisha peke yao bila kutambua kabisa kwamba Kristo anataka kuwaruzuku! Hata ikiwa inaonekana kama hali yako haiwezi kusuluhishwa, au uko kwenye kina kirefu cha nyika na machafuko yanakuzunguka, kumbuka kuwa unaishi huru dhidi ya hali hizo na kwamba ukitambua uwepo wake maishani mwako, atakupa riziki bora zaidi, upendo na utunzwaji.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi bila kujali hali zinazonizunguka! Mungu yu pamoja nami siku zote na tayari amenipa maziwa na asali bila kujali changamoto ninazoweza kukutana nazo! Katika Kristo nina RIZIKI ZILIZO BORA ZAIDI! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 4:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 1 Wafalme 1-2, Zaburi 37, 71, 94



**2 Timotheo 3:16**
**Kila andiko , lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.**

Fikiria juu ya mstari huo kwa sekunde! Maandiko yote yametolewa kwa uvuvio wa Mungu; maana yake ni pumzi ya Mungu. Kisha inasema ni faida, maana yake inakupa faida. Neno zuri kiasi gani!

Kwa hivyo kimsingi, maandiko ni ya mafundisho, kumaanisha yanafundisha na kukuwekea utaratibu. Neno hilo pia ni la kuonya na kusahihisha. Neno kuonya hapo ni epanórthōsis katika Kigiriki, ambalo linamaanisha kurekebisha. Kwa hiyo Neno ni la KUREKEBISHA chochote kinachohitaji kutengenezwa katika maisha na mazingira yako. Je, unaona hilo? Je, umewahi kuona hivyo? Neno halisahihishi tu kasoro za tabia; linarekebisha chochote kingine kinachoenda vibaya kwako ili urejeshwe. Iwe ni maswala ya pesa, maswala ya kiafya, maswala ya uhusiano, n.k. Neno litakuepanórthōsis. Litakurekebisha wewe na chochote kibaya katika maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Nina kirekebisho upande wangu. Ninaweza kutuma Neno kurekebisha matatizo yangu yote. Leo naamka na kutuma Neno kama itifaki kwenye maisha yangu yajayo ili kila kikwazo kirekebishwe kwa Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:28


**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 119

# GOODNEWS TESTIMONIES



**Semi Wara**

24 years ago Semi Wara joined the British Army and served as a soldier. He did tours to Cyprus, Iraq, Afghanistan and also served in Somalia for the British Embassy. Whilst serving on a tour in Afghanistan in 2006, he experienced first-hand, what it was like to fight the Taliban and lost many close friends in this war. He was looking to fill this empty void in him but God always had a plan, and a purpose in his life and that was made possible when he joined Spirit Embassy The GoodNews Church. He has served his country as a soldier for many years but the biggest reward is serving Jesus Christ, and being a soldier in God's army.



**Michelle Mason**

11 years ago Michelle Mason was living a life of sin working as a lap dancer. She used to coordinate private parties at a gentleman's nightclub. She was indulging in a life of alcohol and drugs and her life spiralled drastically out of control. She was lost and broken and had no ability to live a sober life. Years later she became a Christian and left that lifestyle and separated herself from the things of this world. She had a personal encounter with Jesus Christ that made her realise that you are never too far gone, God will call you, appoint you, and work through you to bring Him glory. Through joining Spirit Embassy, God's Word had completely transformed her life.



**Trance Hove**

At the age of seven Trance Hove was introduced to Hip-Hop music. During his teen years the music he listened to as a child had shaped him as a young adult. He then started to hang out with drug dealers, career criminals and violent gangsters in the area he grew up in. He was attracted to the money they were making. Although he was making a lot of money by selling drugs, he had to constantly look over his shoulder. He had to leave this lifestyle and he wanted to use his passion for music to influence and inspire the youth to get involved in what God is doing in this generation. He went from making music that glorified the works of the devil to making music to glorify The Lord Jesus Christ.

# GOODNEWS TESTIMONIES



### Akapusi Qera

Akapusi Qera is a former Fijian professional rugby union player. He came onto the professional Rugby scene in the 2007 World Cup and became the longest serving captain for Fiji. He has travelled the world and won countless trophies and medals for both country and club, however it brings him so much joy knowing where he has come from and where God has taken him. He now uses his platform to reach millions to point people to Christ and bring glory to God, through the teachings of Prophet Uebert Angel.



### Elizabeth Grace

Elizabeth Grace went through a very difficult time in her life when her marriage fell apart. She had to work a full-time job on her own whilst raising a family of five children. As things progressed, it became really challenging for her that she even contemplated ending her life. Whilst going through this ordeal she reached out to some friends who had joined Spirit Embassy The GoodNews Church. After some time she started her own business in healthcare and her business began to grow at an astronomical rate. She became debt-free, and moved into her own home. From living in a council house, eating from a food bank, being unemployed to now owning a successful business and being the employer. She now employs over 70 staff members!



### Richard Edomwonyi

In March 2022 Richard Edomwonyi was involved in a severe car accident which resulted in him having a serious neck and back injury. He was unable to move his neck and had to stay in hospital for some time. A month later he attended the Healing Institute which is the healing ministry and a vehicle that God is using to touch lives in nations, through Prophet Uebert Angel. He was prayed for and immediately in that moment he was completely healed and this was the first time he experienced divine healing in his life.

## USIPOTEZE MUDA, OMBA TU!



**Mathayo 21:22**
**Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini, mtapokea.**

Simulizi la yule mlemavu karibu na bwawa la Bethesda ni mfano kamili wa kuweka mstari wa leo ipasavyo. Bwana Yesu alimwuliza mtu huyo kama alitaka kuponywa . Badala ya kujibu 'ndiyo,' mara moja alianza kulalamika kuhusu jinsi hakuna mtu aliyemsaidia miaka hii yote. Je, Unaikumbuka?

Mtu anayesoma hii leo hufanya hivyo haswa. Analalamika na kunung'unika katika maombi lakini hawaombi kamwe. Mstari wa leo unasema OMBA! Rahisi! Usijisumbue kwa kujaribu kumwelezea Mungu kile kibaya ambacho kimetokea katika maisha yako- kata kwenye mkondo.

Bwana hatakunyima mema kamwe. Kwa hivyo, kuwa na ujasiri wa kufanya maombi yako yajulikane Kwake leo. Omba tu!

## UKIRI WA KINABII

**Ninatabiri kwamba ninayoomba yatatimia upesi . Baba yangu tayari amenipa kilicho bora zaidi, nami nitakiishi na kutembea ndani yake katika Jina la Yesu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 7:11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wafalme 3-4



**Marko 11:23**
**Amini, nawaambia, ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka, ukatupwe baharini; wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo ayasemayo yametukia; yatakuwa yake.**

Katika sayansi kuna aina tofauti au vizio vya nishati. Nishati ya kinetiki ni nguvu katika mwendo inayozalisha matokeo. Pia kuna nishati ya potenshali ambayo ni nguvu ambayo imehifadhiwa tu, kani tuli haitumiki au kujongea. Vile vile, imani isiyotendwa ni nguvu isiyoweza kutekelezwa. Ni sawa na mtu kubeba baruti lakini hajui athari ambayo inaweza kusababisha.

Yesu aliwafunulia wanafunzi wake kwamba hawakuwa na uwezo wa kulaani miti tu bali pia kuhamisha milima kutoka eneo moja hadi jingine. Una mbegu ya imani ndani yako, lakini inaweza tu kutoa matokeo ikiwa utaanza kuitumia. Huenda usianze kwa kuamuru wafu wafufuke, lakini angalau maumivu ya kichwa chako yanapaswa kupona kabla ya kumwomba mchungaji wako akuombee. Tunapokaribia nusu ya mwaka huu wa maziwa na asali, tumia misuli inayoitwa imani leo kwenye biashara, afya au elimu yako. Agiza chochote kinachosimama mbele yako kitokomee bila shaka yoyote. Una roho ya imani, na lo lote utakalolinena litathibitika .

## UKIRI WA KINABII

**Nina roho ya imani ndani yangu; kwa hiyo, ninatamka. Nuru inaangaza katika kila eneo la maisha yangu kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 11:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Mambo ya Nyakati 1, Zaburi 72



**Yohana 15:5**
**Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.**

Inachukua akili ya kawaida kuelewa kwamba damu ambayo inapita katika kichwa chako ni damu sawa na ile inayopita katika mwili wako wote. Ni sayansi ya msingi. Virutubisho vinavyotiririka kwenye shina la mti ndivyo vinavyotiririka hadi kwenye matawi. Kwa hiyo Yesu aliposema, "Mimi ni Mzabibu, na ninyi ni matawi," alimaanisha uzima ule ule ndani Yake ni ule ule unaotiririka ndani yetu.

Ikiwa unataka kuangalia DNA ya Mungu, jiangalie mwenyewe. Unabeba DNA ya Mungu, na hakuna kinachokosekana au kubaki katika hilo. Hakuna hali ambayo ina haki ya kukunyima usingizi wa usiku kwa sababu umezaliwa kutoka juu, na muundo wako wa maumbile unatoka juu. Wewe ni mfano halisi wa utukufu na asili ya Mungu. Kama vile maziwa yanavyorutubisha na kukutunza, ndivyo DNA ya Baba yetu hutunawirisha na kututegemeza!

## UKIRI WA KINABII

**Nimezaliwa kutoka juu na DNA yangu ni ya Mungu. Nimeundwa kwa dutu za Mungu, na hakuna kitakachozuia mafanikio yangu au maendeleo yangu katika mwaka huu wa maziwa na asali. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 4:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Wimbo Ulio Bora



**MWANZO 11:6-7**
**akasema , Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja, na haya ndiyo wanayoanza kufanya; wala sasa hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya,. Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao, ill wasisikilizane maneno wao kwa wao.**

Utamaduni ni mkusanyiko wa imani zinazotawala jamii. Kipengele kimoja muhimu kinachounda msingi wa utamaduni ni lugha. Jamii zote za wanadamu hutumia lugha. Lugha huunda mifumo na mwenendo wetu wa maadili.

Wakati wanadamu walikuwa na lugha moja kwenye Mnara wa Babeli, waliazimia kujenga mnara unaomfikia Mungu. Hata Mungu hangeweza kuwazuia na ilimbidi kuwatawanya kwa kuanzisha lugha mbalimbali. Unapozungumza lugha ya Mungu, kila kitu unachojenga kitasimama. Usichanganye lugha yako kama mtoto wa Mungu na ile inayotoka kwa wale walio duniani. Wanaposema kuna kushuka, utaendelea kusema kuna kuinua. Wanaposema kuna mdororo mkubwa , sema naona maziwa na asali tu! Ongea lugha ya mafanikio, na maisha yako yote yatakuwa na utamaduni wa mafanikio, maendeleo na ushindi.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mbegu ya Mungu na ninaleta utamaduni kutoka kwa Baba yangu (Mungu). Ninasimama juu ya kile ninachoamini, na nitaendelea kunena katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 18:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 1-3



**2 Petro 1:12**
**Kwa hiyo nitakuwa tayari kuwakumbusha hayo siku zote, ijapokuwa mnayajua na kuthibitishwa katika kweli mliyo nayo sasa.**

Tulipokuwa watoto, haikuwezekana kwetu kuelewa dhana fulani za hisabati, sayansi au jiografia kwa sababu akili zetu hazingeweza kuzibeba au kuelewa dhana hizo. Wakati wa kupambanua milinganyo fulani ya hisabati, tulielekea kusema, "Hatuwezi "au "Haiwezekani" kwa sababu ya kutoweza kufahamu wazo hilo. Tulipokomaa vya kutosha, tulielewa kwamba moja toa mbili (1-2) ni swali linalofaa la kihisabati na linaweza kukupa hasi moja (-1).

Vile vile inatumika linapokuja suala la imani. Biblia inazungumza juu ya kuthibitishwa katika ukweli uliopo, ambayo ina maana kuna ukweli uliopita, wa sasa na ujao. Unamkosa Mungu na mawazo yake ikiwa unatembea katika ukweli wake uliopita. Ili uweze kuthibitishwa katika ukweli wa sasa wa Mungu, ni lazima ukae katika Neno, maombi, na ushirika naye. Unapaswa kulishwa katika neno kama vile maziwa yanavyokulisha. Mungu anafanya miujiza, ishara na maajabu ya ajabu katika wakati wetu. Unaweza tu kuwa mshiriki wa hii ikiwa unatembea katika ukweli wa sasa.

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kutembea katika ukweli wa sasa. Njia zangu zimejaa nuru, na sitajikwaa au kushindwa katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Timotheo 2:15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 4-6



**Warumi 10:17**
**Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo.**

Ukristo ndio mfumo pekee wa imani ambao ni wa kisomi. Imani huja kwa kusikia na kusikia Neno la Mungu. Unapata habari ndani yako ili uelewe na kutembea katika nuru ya Yesu Kristo. Kumbuka, Biblia hata inathibitisha kwamba haiwezekani kumpendeza Mungu bila imani. Bila hiyo "sehemu ya imani" ambayo unapata kupitia maarifa, haiwezekani kabisa kumpendeza Mungu.

Kwa maneno ya kimsingi, Ukristo uko mbali na maisha ya wastani. Sisi ndio wenye nuru. Sisi ndio wenye nuru kupitia Neno la Mungu. Ili wewe uitwe mtoto wa Mungu unahitaji maarifa ya kiroho. Inua mabega yako na utembee kwa ujasiri katika eneo la himaya yako. Wewe ni mmiliki wa maarifa ya Ki-Ungu, na kila nyuzi ya nafsi yako imeunganishwa ili kufanikiwa. Unaposoma ibada hii, nuru na maarifa zaidi yanaingia ndani ya roho yako, na hakika utaishi maisha ya ushindi katika Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia. Niko ambaye Niko aliye mkuu anaishi ndani yangu. Mimi ni mtoa nuru kwa kila mtu karibu nami. Haleluya.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 119:130

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 7-9



**Wagalatia 6:17**
**Tangu sasa mtu yeyote asinitaabishe, kwa maana ninachukua mwilini mwangu chapa zake Yesu.**

Chapa ni alama inayoonekana kwa mtu au kitu chochote kisicho hai. Wazo la chapa lilianzia zama za kale ambapo zilitumika kutenganisha kitu kimoja na kingine. Mtume Paulo anasema yeye hubeba chapa au muhuri kama matoleo mengine yanavyoweka. Hali hiyo hiyo inatumika kwangu na kwako : tuna muhuri za Yesu Kristo katika mifumo yetu. Sisi ni wa kipekee katika asili, na inajulikana katika roho kwamba tuna muhuri za Yesu Kristo.

Kuwa na muhuri au chapa ya Kristo inamaanisha Mmiliki wa chapa alikuthibitisha wewe kwenda na kuonyesha wema Wake. Mungu alikuweka chapa na kukuachilia katika ulimwengu huu ili kuonyesha utukufu wake. Songa mbele na uonyeshe utukufu wa Yule ambaye umebeba muhuri yake, katika Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Mihuri ya Kristo iko katika maisha yangu yote. Nilizaliwa ili kuonyesha utukufu wake kwa ulimwengu huu. Kila kitu kunihusu kitakuwa kama maziwa na asali kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Ezekieli 46:16

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 10-12



**Yohana 6:63**
**Roho ndiyo itiayo uzima ; mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima.**

Unapozungumza, unatuma mawimbi katika angahewa, na maneno hayo yanaishi ili kutimia. Ulimi wako hauachii maneno tu bali muundo wa uzima na mauti au mafanikio na kushindwa. Ulimi wako sio tu msuli mdomoni mwako bali ni muumbaji wa hatima. Upo hapo ulipo kwa sababu ya jinsi ulivyotumia ulimi wako, iwe chanya au hasi. Unaposema, "Mambo ni magumu." neno hilo litaenda na kukusubiri ili kuhakikisha kuwa kila kitu kuhusu wewe kitakuwa kigumu sana.

Yesu alisema maneno aliyosema hayakuwa maneno tu bali roho na uzima. Kuwa na vipindi vyako vya mazungumzo kuanzia leo, ukiongea maneno chanya. Mafanikio, afya na ustawi (yaani; maziwa na asali) vyote ni vyako. Hali yako haipaswi kuamua kile unachosema. Badala yake, acha kinywa chako kitengeneze hali unayotamani.

## UKIRI WA KINABII

**Kinywa changu ni kalamu ya mwandishi stadi. Hatima na himaya zinanitokea. Mafanikio, amani na ustawi vyote ni vyangu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Ayubu 22:28

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 13-15



**Isaya 12:3**
**Basi, kwa furaha mtateka maji katika visima vya wokovu.**

Unapopanda ndege, nauli ya tiketi yako haijumuishi tu mwendo wako kutoka eneo moja hadi jingine. Ni kifurushi kamili kwa safari nzima. Inahusisha chakula chako, kila aina ya usaidizi, burudani, faraja na wepesi. Hii inaonyesha kuwa ulipolipia tiketi yako, ulilipia kifurushi kamili ambacho kinashughulikia kila kitu, hakuna kinachokosekana au kupungua. Kadhalika ndivyo ilivyo linapokuja suala la wokovu; ni kifurushi kamili kinachokuja na kila jambo jema linalohusu maisha hadi unyakuo.

Nabii Isaya alisema tuchote kutoka kwenye "visima" vya wokovu. Biblia haisemi 'kisima' bali 'visima' kwa wingi, ambayo ina maana kwamba kuna kisima cha fedha, afya, akili na yote. Unaposoma Biblia, gawa kwa usawa wakati na juhudi zako za kiroho kwa kila eneo na pembe zote za maisha yako. Hakuna kitu kinachopaswa kukosa kabisa katika maisha yako. Leo, simama kwenye haki yako kama mtoto wa Mungu na udai yote yaliyo yako katika Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Afya, mafanikio, ustawi na uwezo vyote ni vyangu na familia yangu . Hatutakosa maziwa na asali katika Jina la Yesu Kristo. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 1:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 16-18



**Yoeli 3:10**
**Yafueni majembe yenu yawe panga, na miundu yenu iwe mikuki; aliye dhaifu na aseme, Mimi ni hodari.**

Maneno tunayosema yanatokeza mawimbi ya sauti na masafa ambayo hubeba roho waovu au malaika kwenye kazi zao. Kila chombo cha kiroho kinahitaji wimbi la sauti kutolewa kupitia maneno ili kusonga. Maneno unayozungumza kila siku yanaunda njia kuu na njia katika roho za kusafirisha malaika au mapepo. Nguvu katika roho husogea kupitia mawimbi na masafa yanayotokezwa na maneno hayo. Unapokuja kwa mchungaji na kuomba "neno," unachoomba ni masafa kusafirisha vitu vizuri maishani mwako.

Nabii Yoeli alitoa mkakati wa wazi kabla ya vita vya Israeli. Alitangaza, "aliye dhaifu na aseme, Mimi ni hodari." (Yoeli 3:10). Maneno hayo yangekuwa nguvu yao wakati wa vita. Leo, unaweza pia kutangaza kwa kinywa chako kuwa wewe ni hodari, tajiri na umefanikiwa. Maneno hayo ni masafa ya wewe kufanikiwa maishani. Haijalishi unajisikia nini mwilini mwako au salio lako la benki linasema nini, sema tu, "Nina nguvu, tajiri na nimebarikiwa!" Utavuna mavuno mengi mwaka huu kwa Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Nina nguvu, nina uweza na nimefanikiwa. Ninaishi juu ya mipaka yote ya ulimwengu huu kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 13:5b-6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 19-21



**WARUMI 10:17**
**Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo.**

Katika ulimwengu wa roho, unakuzwa na ujuzi unaopata. Maandiko yetu yanatuonyesha kwamba imani au uwezo wowote wa kiroho huja kupitia kusikia habari fulani. Inaonekana kama kiasi cha maarifa ulicho nacho kuhusu Mungu ni sawa na mlima wa imani unaoubeba. Imani dhaifu ni matokeo ya maarifa duni ya Kristo. Neno la Mungu huimarisha misuli ya kusogeza milima yote unayoiona mbele yako.

Lisha Neno la Mungu na ukue misuli yako ya kiroho. Biblia yako ni kama sehemu yako ya mazoezi ya Roho Mtakatifu: kila kitu kipo kukufanya kuwa jitu la kiroho. Utaelewa kanuni za ajabu ambazo zitashtua ulimwengu unaokuzunguka. Kusanya Neno; kua katika neema na katika kumjua Yesu Kristo. Tafuta njia za kukua na kuzaa matunda katika maeneo mbalimbali ya maisha yako, kiroho na kimwili na hakika utaona maziwa na asali vikifurika!

## UKIRI WA KINABII

**Maarifa ya Mungu yanakua ndani yangu. Njia zangu zimejaa nuru na utukufu. Ninamiliki mali zangu zote kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 10:23

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 22-24



**Zaburi 69:30**
**Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo, nami nitamtukuza kwa shukurani.**

Unapomtukuza Mungu, maana yake unazieleza shida zako na mazingira yako jinsi Mungu wako alivyo na nguvu. Kufanya maombi ambapo unamsimulia Mungu shida zako si chochote bali ni mazungumzo ya njia moja ambapo Mungu husikia shida zako tu. Kumtukuza au kumuinua Mungu ina maana kwamba tunarudi kwenye matatizo haya yote na kuyaambia kuhusu Mungu wetu. Sasa hivi, una Mungu anayejua masuala yako, lakini masuala yako hayamjui Mungu wako.

Tunabadilisha mchezo leo. Uambie ugonjwa huo mwilini mwako kuwa Mungu wako ni mponyaji. Iambie hiyo roho ya umaskini kuwa Mungu wako ni mpaji, na iambie hiyo hali ya kukatisha tamaa akilini mwako kwamba Mungu wako anaweza kukuinua kutoka mavumbini na kukuweka mahali pa juu ili kula pamoja na wafalme. Zivamie na kugandisha nguvu za kila tatizo katika maisha yako kwa kumtukuza Mungu na kutangaza ukuu wake kwa kila hali.

## UKIRI WA KINABII

**Mungu wangu ni mkuu na mwenye nguvu; Anakaa katika mduara wake Mwenyewe. Yeye ni Mtukufu, na Anashikilia kila kitu mkononi Mwake. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Matendo 16:25

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wafalme 5-6, 2 Mambo ya Nyakati 2-3



**Kumbukumbu la Torati 1:6**
**BWANA, Mungu wetu, alituambia huko Horebu , akasema, Mlivyokaa katika mlima huu vyatosha.**

Maji yaliyotuama ni mazalia ya kila aina ya bakteria na magonjwa ambapo wanazaliana kwa uhuru na kupanua himaya zao. Mungu anachukia kudumaa kwa sababu kunazaa chuki, dharau na vita. Wenye chuki wengi sio watu waliofanikiwa bali ni wale ambao wana maisha yaliyodumaa bila kusonga hata kidogo. Watu waliofanikiwa wana shughuli nyingi za kusonga mbele na hawana wakati wa kutazama mambo ya watu wengine.

Biblia inasema tunasonga kutoka utukufu hadi utukufu, ambayo ina maana kwamba kutembea kwetu kwa imani ni mjongeo. Hatuko palepale. Miujiza tuliyoiona juma lililopita si kitu ukilinganisha na kile tutakachokuwa tunakiona leo na kesho. Tunabadilika katika viwango vya utukufu kila wakati. Mimi binafsi nilipitia. Baada ya kujaza viwanja vya michezo na kufanya kila aina ya miujiza, baba yangu, Mchungaji Chris, aliniambia, “Ulichoona hapo awali ni mchezo wa mtoto.” Lo! Hiyo ina maana kuna utukufu mkuu zaidi unakuja; hiyo inakuhusu pia. Unaposoma ibada hii, utukufu mkuu zaidi, aina ya maziwa na asali, unakujia sasa hivi!

## UKIRI WA KINABII

**Ninasonga kutoka utukufu hadi utukufu. Maisha yangu ni ya mjongeo na kila siku nitaona miujiza na shuhuda mpya kabisa kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 3:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 1 Wafalme 7, 2 Mambo ya Nyakati 4



**1 Timotheo 4:15**
**Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote.**

Yesu, katika wakati wake, aliendа kwa kiasi kikubwa kuwaambia wasikilizaji wake kwamba kama hawataamini ujumbe wake, angalau wanapaswa kuamini miujiza anayoifanya. Miujiza ni nini? Ni uthibitisho wa kile tunachoamini. Injili haiko katika maneno tu bali katika udhihirisho wa nguvu. Nguvu inapodhihirika , inatoa uthibitisho unaoonekana.

Biblia inafunua katika mstari wa leo kwamba tukitafakari sheria za Mungu, haitaishia hapo , bali faida yetu itaonekana kwa wote. Unaweza kuzungumza na Mungu kwa faragha, lakini udhihirisho Wake utakuwa wazi sana. Unaposoma neno hili na kulitafakari, roho yako inashika kitu ambacho kitadhihirika katika afya yako, biashara, elimu na kila eneo la maisha yako. Wewe ni Mkristo mtoa ushahidi. Maisha yako yatashibishwa na kuwa matamu kama maziwa na asali!
Leo utaona uthibitisho wa unayoyaamini!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni Mkristo mzalisha uthibitisho. Nitaishi muda mrefu wa kuona utukufu wa Mungu ukidhihirika katika maisha yangu. Haleluya.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 4:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 1 Wafalme 8, 2 Mambo ya Nyakati 5



**Waebrania 6:10**
**Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata sasa mngali mkiwahudumia.**

Andiko letu hapo juu linatoa ufafanuzi wa kimsingi wa udhalimu, ambao huenda wengi hawataki kuusikia. Bado, unasaidiwa tu pale ujinga wako unapokabiliwa. Biblia inasema kwamba Mungu si " dhalimu " hata aisahau, kumaanisha kwamba ikiwa Angesahau, angekuwa "dhalimu." Kulingana na andiko hili, kila mtu anayesahau jambo jema alilotendewa ni "dhalimu." Hakuna njia mbili juu ya hili.

Kuna kaka au dada ambaye alikusaidia hapo awali, huduma ambapo ulilishwa na kusaidiwa, au hata mfanyakazi wa chini ambaye angeweza kukusaidia. Chukua muda leo kuwathamini. Piga simu, tuma ujumbe mfupi au tafuta njia ya kuonyesha shukrani zako. Hata neno la fadhili linatosha kuthamini mtu. Chagua kuwa mwadilifu kwa kutosahau matendo mema ya watu wengine waliyofanya katika maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Nina haki ya Mungu, na sitawasahau wale walionitendea mema. Ninaifanya kuwa utamaduni wangu kuheshimu na kuthamini wasaidizi wa hatima yangu, katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 5:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Mambo ya Nyakati 6-7, Zaburi 136



**Luka 18:1**
**Akawaambia mfano , ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa;**

Sensa inachukuliwa kuwa hesabu rasmi au uchunguzi wa idadi ya watu. Nchi nyingi hufanya sensa yao mara kwa mara ili kunasa aina tofauti za data. Inasaidia nchi kupata maarifa ya jumla kuhusu muundo wa idadi ya watu, idadi ya watu, mapato, n.k. Pia kuna sensa ya mbinguni ambayo wengi hawaijui, na maandiko yetu leo yanafunua jambo kuhusu hilo.
" imewapasa kumwomba Mungu"

Kwa maneno rahisi, kulingana na andiko hili, unapaswa kuwa mtu wa kuomba ili kuchukuliwa kuwa mtu kwa Mungu. Mwanadamu pekee ndiye anayeweza kuomba. Wale ambao hawafanyi maombi kwa Mungu hawachukuliwi sehemu ya idadi yake. Ni kupitia maombi yako ndipo unapoandikwa katika daftari la wanadamu katika ulimwengu wa roho. Mungu anataka ushirika nawe kwa njia ya maombi. Ikiwa huombi, wewe ni kitu tu ambacho kinajongea tu huku na huko katika uso wa Dunia. Fanya maombi kuwa mtindo wako wa maisha, na utahesabiwa na Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Nitaomba na sitazimia. Maombi yangu yatainuka kama uvumba kila siku. Ushirika wangu na Mungu ndio kila kitu, nami nitapata maziwa na asali bora zaidi ya Mungu katika Jina la Yesu!**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wathesalonike 5:16

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Zaburi 134, 146-150



**2 Wakorintho 5:17**
**Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama, yamekuwa mapya.**

Wakristo wengi bado wamekwama katika ufahamu wa kale wa Kristo kufa kwa ajili yetu, wakiamini kwamba walimfanya achubuliwe na kusulubiwa msalabani. Inasikitisha jinsi Mwili wa Kristo unavyonunua ufahamu huu wa zamani, wa kawaida. Kwa kweli, ni kinyume cha Maandiko kwetu kuamini sisi ndio sababu ya kifo cha Yesu Kristo. Sisi sio sababu ya kifo cha Kristo bali ni matokeo ya ufufuo wake. Hatukusababisha Yesu kuteswa na kusulubiwa; tuliibuka kama matokeo ya yote hayo.

Maandiko yetu yanasema mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya. Neno 'mpya' ni la Kigiriki kainós , ambalo linamaanisha kitu ambacho hakijawahi kuwepo hapo awali. Huwezi tena kuhesabiwa kati ya wale waliosababisha Kristo kufa kwa sababu wewe ni aina mpya kabisa ya kiumbe! Tembea katika ufahamu kwamba wewe ni kiumbe kipya kisicho na uhusiano na dhambi au dosari zako zilizopita. Kubali mwanzo mpya na fursa mpya unapopitia mwaka wa maziwa na asali!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiumbe kipya katika Yesu Kristo na kila kitu kunihusu ni kipya. Hakuna alama ya dhambi, umaskini au kushindwa ndani yangu, katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wafalme 9, 2 Mambo ya Nyakati 8



**Marko 6:5**
**Wala hakuweza kufanya mwujiza wowote huko, isipokuwa aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya .**

Desturi ni uhamishaji wa imani na mila kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ni mafanikio yaliyogandishwa. Watu wameunganishwa na mila, nzuri au mbaya, na chochote wanachokuwa ni matokeo ya hii. Biblia inatuambia Yesu hakuweza kufanya muujiza wowote mkubwa alipoenda katika nchi yake. Kumbuka Biblia haikusema hakufanya , bali " hakuweza ," ambayo ina maana kwamba alijaribu na kushindwa. Ingawa alikuwa Mungu katika mwili, kuna mambo ambayo alishindwa kufanya kwa sababu ya mapokeo. Walilifanya Neno la Mungu kuwa lisilo na nguvu kwa mifumo yao ya imani.

Leo ni siku mpya. Ni wakati wa kwenda kinyume na aina zote za desturi hasi. Amini kila kitu ambacho Mungu anasema bila kivuli cha shaka. Ikiwa Anasema pesa zinakuja, hakika zinakuja. Wakati ulimwengu unatangaza kwamba utaishi hadi umri fulani, tengeneza mtindo mpya wa mapokeo ya Ki-Mungu katika kizazi chako, na ujulishe ulimwengu unaishi muda mrefu zaidi ili kutangaza wema wa Bwana.

## UKIRI WA KINABII

**Aina zote mbaya za desturi katika damu yangu zimevunjwa leo. Ninamwamini Mungu kwa jambo kuu zaidi katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 7:13

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 25-26



**Mwanzo 13:15**
**maana nchi hii yote uionayo nitakupa wewe na uzao wako hata milele .**

Bwana alisema jambo la kina sana kwa Ibrahimu, " yote uionayo nitakupa wewe." Kuna kipengele cha kuona katika imani. Ikiwa unaweza kuiona, unaweza kuwa nayo. Ibrahimu alitakiwa kupewa kiasi ambacho angeweza kufikiria. Kuzungumza kwa kawaida, ilikuwa vigumu kwa Ibrahimu kuona pengine zaidi ya kilomita mia mbili . Kwa hiyo, Mungu alikuwa akimwita kwenye ulimwengu wa mawazopicha. Ibrahimu baadaye alimiliki karibu kila kipande cha uso wa dunia, maana yake alipoambiwa aone , hakutumia macho yake ya kimwili tu, bali yale ya kiroho.

Usizuiliwe na hali yako au dosari zozote za kimwili ndani ya kipenyo chako. Ona zaidi ya asili, na ujue kwamba kadiri unavyoweza kuona, unaweza kumiliki. Adui anaweza kujaribu kuweka vipofushaji karibu nawe ili usione zaidi ya mdororo, magonjwa, au umaskini, lakini Neno hili linafungua macho yako kuona mbali zaidi. Utashuhudia maziwa na asali katika kila eneo la maisha yako!

## UKIRI WA KINABII

**Sizuiliki kwa neema ya Bwana wetu Yesu Kristo. Kupitia neema, ninaona zaidi ya mwili wangu katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 4:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 27-29



**Wagalatia 4:19**
**Vitoto vyangu, ambao kwamba ninawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu.**

Katika taasisi za elimu za kidunia, ukifeli moduli au darasa, huruhusiwi kuhitimu au kwenda ngazi inayofuata. Ni mfumo unaosimamia viwango vya elimu ili kuzalisha wanafunzi bora. Katika chuo kikuu cha Mungu, pia huwezi kuruka madarasa. Lazima upitie moduli zote hadi ufikie kiwango fulani. Ikiwa na maana kwamba unapaswa kurudia, unapaswa kufanya hivyo hadi uhitimu. Unapowaona majenerali wa Mungu unaowafurahia, kumbuka hawakutokea juu tu, bali walipitia madarasa ya kila namna mpaka kufikia kiwango hicho.

Paulo anazungumza juu ya Kristo kuumbika kikamilifu ndani yako. Hii inaonyesha kwamba kuna baadhi ya Wakristo ambao wanaweza kuwa na sikio la Yesu tu bila mwili wake kamili . Kua kupitia Neno, hatua kwa hatua , mpaka Kristo amekamilika ndani yako. Unapokua, utaona matokeo yote unayotaka yakitimia . Chukua muda kukua hatua moja na ngazi moja hadi uwe jitu la kiroho.

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kukua hatua kwa hatua kupitia Neno la Mungu. Roho yangu iko tayari na inasukumwa kushika Neno la Mungu. Ninakua kutoka utukufu hadi utukufu katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 3:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mhubiri 1-6



**Mathayo 25:23**
**Bwana wake akamwambia, Vema, mtumwa mwema na mwaminifu, ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.**

Tukifika Mbinguni, Mungu hatakuuliza kuhusu miujiza aliyokufanyia. Wala hatakuuliza juu ya kiasi gani ulichofaidika na neema na rehema zake. Hapana, atakuuliza kuhusu ulichofanya kwa neema na Ukristo aliokupa. Anajali zaidi jinsi unavyopata faida katika ulimwengu huu ukiwa bado duniani. Mwisho wa yote ni kile utakachowasilisha mbele ya Bwana ukifika Mbinguni. Je! Atasema, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu?" au Ataona mtu aliyekuwa akilia na maombi kila siku?

Tumia wakati huu kwa faida kuleta nuru kwa familia yako, wafanyakazi wenzako na kila mtu karibu nawe. Okoa roho kwa kushirikisha Neno au kuhimiza mtu kuwa kanisani. Uko hapa kwa sababu, kwa hivyo kumbuka kuwa makini hadi mwisho. Unahitaji kuondoka katika ulimwengu huu na kitu cha kuwasilisha mbele ya Bwana ili uweze kutangazwa kuwa mtumishi mwema na mwaminifu.

## UKIRI WA KINABII

**Nimezaliwa na niko tayari kufanya utumishi wa Bwana wangu. Nafsi zitaokoka kupitia mimi. Mimi ni muhudumu wa upatanisho katika Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 3:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mhubiri 7-12



**2 Wakorintho 4:9**
**twaudhiwa, bali hatuachwi; tunatupwa chini, bali hatuangamizwi;**

Paulo alitaja aina zote za udhia unaotujia sisi kama watoto wa Mungu. Lakini jambo zuri zaidi alilosema ni kwamba hatuharibiwi au kumalizika. Wakati ulimwengu unatushinikiza, wanapaswa kujua tumeumbwa kwa nini . Tumezaliwa kwa Roho, na tunakula Neno la Mungu. Neno ni vinasaba vyetu. Tunda la embe likikamuliwa, kinachotoka ni juisi ya embe. Ni vile vile kwa matunda mengine yoyote pia.

Unapokamulia na changamoto za maisha haya, kinachopaswa kutoka kwako ni "juisi ya Neno" kwa sababu tumeundwa na Neno la Mungu. Hakuna kitakachokutikisa wewe au familia yako kwa sababu umekita mizizi katika Neno Lake. Umesimama juu ya Kristo Mwamba imara, na hakuna mafuriko wala mateso yatakayokutikisa kwa Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Nimeundwa na Neno la Mungu kwa sababu najilisha Neno la Mungu kila wakati. Sitatikisika wala sitaondoshwa kwa sababu ninalo Neno ndani yangu . Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 4:4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 1 Wafalme 10-11, 2 Mambo ya Nyakati 9



**Mathayo 5:16**
**Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni**

Linapokuja suala la bidhaa, tarehe za mwisho wa matumizi huashiria tarehe ambayo kitu hakiwezi kuliwa au kutumika tena. Ni mwisho wa uhalali wa kitu. Muda au mazingira yanaweza kusababisha kitu kuisha muda wake. Kwako wewe kama mtu, kuna nguvu ambazo zinataka uishe. Hii ndiyo sababu tuna watu wa Mungu, huduma, biashara au himaya ambazo hapo awali zilikuwa na nguvu sana, lakini sasa yote ni historia. Walilazimishwa kuisha muda wao na nguvu zinazotawala ulimwengu huu.

Biblia inasema ninyi ni nuru ya ulimwengu huu. Wajibu wako ni kuendelea kuangaza hadi Yesu Kristo arudi. Acha nuru yako iangaze na kamwe usiifiche. Kataa kuisha muda wako na uthibitishe unabii wa maziwa na asali kuwa wa kweli. Unapowasiliana na Mungu kupitia Neno hili na maombi, kila kitu kukuhusu kinahuishwa . Kila kitu kuhusu wewe kitastahimili mtihani wa muda, na hautaisha kwa Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Nimezaliwa kutoka juu . Nishati ya Mungu iko ndani ya roho, nafsi na mwili wangu. Nitaendelea kuwasha moto tena na sitaisha muda wangu kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Timotheo 4:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: Mithali 30-31



**Wagalatia 2:2**
**Nami nalikwenda kwa kuwa nalifunuliwa, nikawaeleza Injili ile niihubiriyo kati ya Mataifa, lakini kwa faragha kwa hao watu wenye sifa, isiwe labda napiga mbio bure au nalipiga mbio bure.**

Mtume Paulo anatupa siri ya mafanikio katika mstari huu. Akasema, "nalikwenda kwa kuwa nalifunuliwa." Ufunuo ni ufunguzi wa macho, au kwa usahihi zaidi, kuondolewa kwa mizani. Mafanikio ni zao la ufunuo ulio nao. Paulo anahusisha mkakati wa wazi wa kuinuliwa: alipanda kwa ufunuo, akitujulisha kwamba ni ufahamu wako wa Neno ambao huamua urefu wako katika maisha.

Pesa, afya, na biashara yako vyote vimeambatanishwa na ufunuo ambao umepokea. Kupata ufunuo ni mkakati wa kuinuka. Nenda kwenye Neno, nawe utarudi na ushuhuda! Unapozama ndani zaidi katika Neno la Mungu, hata kuanzia leo, nuru ya ufunuo inakujia, na kuinuliwa ni hakika. Lifanye Neno kuwa kiwango chako cha kuinuliwa. Maziwa na asali ulikuwa unabii wako uliotangazwa, shikamana nao! Jitoe kwa Neno, ambalo Biblia inaliita neno la unabii lenye uhakika zaidi, na maisha yako hayatakuwa sawa tena.

## UKIRI WA KINABII

**Neno la Mungu ndilo kipimo changu cha kuinuka. Nimewekewa alama ya ukuu na mafanikio katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 4:20-23

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wafalme 12-14



**Waamuzi 6:12**
**akamtokea , akamwambia, BWANA yu pamoja nawe, Ee shujaa .**

Mungu anakujua zaidi ya unavyojijua. Anafahamu zaidi ustawi wako kuliko wewe. Biblia inasema Gideoni alikuwa akijificha mbele ya Wafilisti, ambao walikuwa wakija kila mara kuteka nyara na kuchukua mavuno kutoka kwa Waisraeli. Kujificha kwa Gideoni ilikuwa ishara wazi ya woga na hofu, lakini Mungu hakuzungumza naye kulingana na jinsi Gideoni alivyohisi au kujiona. Badala yake, Mungu alimwita vile Alimjua Gideoni kuwa: "ewe shujaa. "

Gideoni lazima alijiuliza, Mungu anawezaje kuniita shujaa, ilihali ninajificha dhidi ya adui ? Jibu ni kwamba Mungu anapokutazama, anaona zaidi ya kile unachokiona. Unaweza kujiona wewe ni nyota anayechipukia au mtu unayejaribu kujikimu tu, lakini Mungu anakuona wewe ni suluhisho la matatizo ya nchi yako. Wewe ni jitu, kulingana na Mungu. Kwa hivyo, usiruhusu mazingira yako, historia, au hali ya elimu kukupambanua. Ulizaliwa ili kushinda kwa Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtu hodari wa ushujaa . Nina nguvu kutoka juu na ulimwengu bado haujaona kitu kikubwa na chenye nguvu kikitoka ndani yangu kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 2:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Mambo ya Nyakati 10-12



**Mithali 18:21**
**Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi, nao waupendao watakula matunda yake.**

Unapotamka maneno, kumbuka hayo si maneno tu yanayotoka kinywani mwako na kusambaa kwenye hewa nyembamba. Maneno unayotamka yana uwezo wa kutengeneza maisha yako kuwa bora au mabaya zaidi. Ndiyo sababu unahitaji kuweka thamani kwenye maneno unayozungumza. Weka kiwango kwenye maneno yanayotoka kinywani mwako. Hii haina uhusiano wowote na nafasi yako ya kihemko. Yote ni kuhusu kuchora mwendo wa maisha yako kwa maneno yako. Maziwa yote na asali unayotaka viko katika uwezo wa ulimi wako.

Leo, chagua kutamka uzima, amani, na ustawi. Usiruhusu hisia au hali yako ya sasa kubadilisha lugha yako. Wakati mambo ni mazuri au si mazuri, sema mambo chanya bila kujali ni nini. Hatima yako inakungoja uongee yale yenye tija. Ulimi wako ni silaha ya kupanga maisha yako yajayo. Tamka na tangaza maziwa na asali katika siku yako, na hakika utaona udhihirisho wa neno hilo.

## UKIRI WA KINABII

**Ninaamuru na kutangaza ustawi katika kila eneo la maisha yangu. Nitaishi maisha ya maziwa na asali kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 12:36-37

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wafalme 15, 2 Mambo ya Nyakati 13-16



GoodNews DAILY



**Warumi 5:5**
**Na tumaini halitahayarishi ; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.**

Wito wa upendo si amri kwetu sisi ambao ni Wakristo wa agano jipya. Hatuendeshi mambo kwa sheria na amri. Upendo ndio asili yetu. Kuhusu mimi na wewe, neno letu linapatikana katika andiko hapo juu, "pendo la Mungu limemiminwa katika mioyo yetu." Hatupendi kwa amri bali kwa asili. Mioyo yetu imejaa upendo. Tumezama katika upendo wa Yesu; kwa hiyo, hatuhitaji kuamriwa kupenda. Unatoka tu kwa kawaida kama kupumua.

Chagua kupenda na kuwa mhudumu wa upatanisho kwa familia yako na marafiki. Hakuna nafasi ya kuweka kinyongo au uadui. Yesu Kristo anarudi, na hakuna wakati wa michezo na shida. Upendo katika mambo yote na siku zote; hiyo ndiyo asili ya mtu ambaye moyo wake umemiminwa kwenye upendo na Bwana wetu Yesu Kristo.

## UKIRI WA KINABII

**Napenda, si kwa amri, bali kwa asili. Leo na kila siku, ninachagua kupenda na kufanya amani na kila mtu karibu nami. Ninaondoa chuki na uadui kwa Jina la Yesu.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 4:8; Yohana 3:16

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Maandiko yako ya leo: 1 Wafalme 16, 2 Mambo ya Nyakati 17



**Matendo 17:28**
**Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu; kama vile mmoja wenu mtunga mashairi alivyosema, Sisi sote tu wazao wake.**

Unapogonga ukuta, utajeruhiwa na hata kuwa na michubuko mingi kutokana na athari. Lakini ukiingia kwenye tingatinga, utaponda kuta zote chini na kupita. Ikiwa uko ndani ya tingatinga, unajua hakuna kizuizi chenye nguvu za kutosha kusimamisha juhudi zako. Biblia inatuambia kwamba tunaishi, tunatembea na kuwa na uhai wetu ndani ya Yesu. Hii inatuambia kwamba Yesu si mtu tu bali ni mahali . Yesu ni eneo letu, na tunasonga ndani ya mazingira yake.

Uko ndani ya Mtu mkuu kuliko tingatinga lolote. Hakuna kinachoweza kukuzuia. Biashara yako haiwezi kukataliwa na mtu yeyote kwa sababu uko ndani ya Nguvu kubwa zaidi. Kila kitu kuhusu wewe hakika kitakuwa na kifungu laini kwa sababu unasonga katika mazingira bora zaidi, Bwana Yesu Kristo. Ndani Yake, wewe haushindwi na hauguswi. Kila kitu kinatiririka kama maziwa na asali unapokaa katika mahali bora zaidi ambalo ni Bwana Yesu Kristo!

## UKIRI WA KINABII

**Kristo ndiye mahali pangu. Katika Yesu Kristo ninaishi, ninatembea, na kuwa na uhai wangu. Siwezi kuzuilika kwa sababu niko ndani ya mamlaka kuu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 5:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wafalme 17-19



**Zaburi 119:130**
**Kufafanusha maneno yako kwatia nuru; na kumfahamisha mjinga.**

Neno Illuminati linahusishwa na jamii ya siri ya watu wanaodai kujua zaidi kuliko binadamu wa kawaida . Je, Illuminati halisi ni akina nani? Jina lao linatokana na illumination, ambalo lina maana ya waleta mwanga. Biblia inasema kuingia kwa Neno la Mungu huleta nuru, na Mungu mwenyewe alituambia tuache nuru yetu iangaze. Hiyo ina maana sisi ndio waleta nuru halisi. Sisi ni nuru katika ulimwengu huu!

Dunia si kitu bila sisi, nuru halisi. Sisi ndio Illuminati halisi, waletaji wa nuru kwa ulimwengu huu. Wakati ulimwengu hauna tumaini, tunaleta tumaini na imani kupitia ujuzi wa Yesu Kristo. Leo, kupitia Neno la Mungu, nuru yako inaongezeka, na majibu yote ya familia yako yatapatikana ndani yako. Aliye ndani yako ni mkuu kuliko aliye katika dunia. Nenda nje ukaonyeshe utukufu wa Mungu . Wewe ni mchanganuo wa kweli wa Mungu, katika Jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ndiye mleta nuru halisi. Ninamiliki uwezo kutoka juu, na kila kitu kinachonizunguka kina nuru. Njia zangu zinang'aa na kuleta maziwa na asali kwa Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 5:14

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 1 Wafalme 20-21

## ZAIDI YA HEKIMA YA WANADAMU



**1 Wakorintho 3:19**
**Maana hekima ya dunia hii ni upuzi mbele za Mungu. Kwa maana imeandikwa, Yeye ndiye awanasaye wenye hekima katika hila yao.**

Hekima ni sifa ya kuwa na uzoefu, ujuzi na uamuzi mzuri. Ulimwengu una viwango vyake vya kuamua kiwango cha hekima cha mtu. Wakati mwingine hupimwa kwa kiwango cha fedha, sifa za elimu au ushawishi katika nyanja mbalimbali za maisha. Maandiko yetu ya leo yanafunua kwamba kuna hekima ya juu ambayo ni zaidi ya eneo la ubinadamu. Kadiri tunavyoona uvumbuzi wote kwenye sayari hii, bado kuna hekima inayozingatiwa kuwa ni bora zaidi.

Mtume Paulo anasema hekima ya ulimwengu huu ni upumbavu. Huhitaji kuamini au kutegemea mifumo ya dunia hii kwa sababu siku zote ina mapungufu . Mungu pekee ndiye kielelezo cha hekima kuu. Kwa hekima yake, aliweka misingi ya dunia na akaamuru kila kitu kiwe katika nafasi yake. Unapotafakari Neno hili na kuomba, hekima hiyo hiyo inapenya kwenye roho yako. Utatenda kwa hekima ya juu zaidi ambayo haiwezi kushindwa, kwa Jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Nina hekima kutoka juu. Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia. Matunda ya kazi yangu yamebarikiwa kwa Jina la Yesu. Amina.**

### MAFUNZO ZAIDI
Yakobo 1:5

### MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365
Maandiko yako ya leo: 1 Wafalme 22, 2 Mambo ya Nyakati 18



**Yohana 18:37**
**Basi Pilato akamwambia, wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, wewe wasema kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili haya, na kwa ajili ya haya nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu.**

Fokasi ni kipengele muhimu cha mafanikio. Unapojua ni kwa nini unapumua dakika hii, umakini wako hubadilika kuelekea mambo ambayo ni muhimu zaidi. Yesu alimwambia Pilato, "kwa ajili ya haya nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli." Alijua ni kwa nini Alikuja katika ulimwengu huu, na Aliendelea kuzingatia jambo hilo kwa karibu miaka mitatu. Matokeo yake, ushawishi Wake bado unazungumziwa hadi leo.

Chagua kile ambacho ni muhimu katika maisha. Zingatia mambo yenye faida kwa Ufalme. Hakuna nafasi tena ya mazungumzo ya bure bure, shida na chuki. Ni wakati wako wa kukimbia na Habari Njema ya Bwana wetu Yesu Kristo kabla ya ndege ya kwanza kuruka (yaani, unyakuo au ufufuo wa watakatifu). Tumia wakati wako kwa busara: fokasi! Familia yako, huduma na biashara zote zinakungoja. Ni wakati wa kuzingatia yale mambo ambayo yana faida kwako na kwa Ufalme.

## UKIRI WA KINABII

**Nilizaliwa ili kutangaza Habari Njema ya Yesu Kristo. Wengi wataona nuru kupitia kwangu. Fokasi yangu ni kwa Kristo hadi unyakuo, katika Jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yakobo 1:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365**
Andiko lako la leo: 2 Mambo ya Nyakati 19-23


GoodNews
DAILY
"A GLOBAL VISION REQUIRES A GLOBAL BUDGET, BECOME A GOODNEWS DAILY PARTNER TODAY"
PROPHET
UEBERT ANGEL
www.goodnewsworld.com/gndpartner
GoodNews Daily Devotional
@goodnewsdailydevotional

# JE, TAYARI UMEMPOKEA YESU KRISTO?

TUNAKUALIKA KUMFANYA YESU KRISTO KUWA BWANA WA MAISHA YAKO KWA KUOMBA OMBI HII;

"Ee BWANA MUNGU, NINAKUJA KWAKO KATIKA JINA LA YESU KRISTO. NINAAMINI KWA MOYO WANGU WOTE KATIKA YESU KRISTO MWANA WA MUNGU ALIYE HAI. NAAMINI ALIKUFA KWA AJILI YANGU NA MUNGU AKAMFUFUA KUTOKA KWA WAFU. NAAMINI YUPO HAI LEO. NINAKIRI KWA KINYWA CHANGU KWAMBA YESU KRISTO NDIYE BWANA WA MAISHA YANGU TANGU LEO.KATIKA YEYE NA KWA JINA LAKE NINA UZIMA WA MILELE, NIMEZALIWA UPYA. ASANTE BWANA KWA KUIOKOA NAFSI YANGU. MIMI SASA NI MTOTO WA MUNGU. HALELUYA!"

HONGERA SANA!
SASA WEWE NI MTOTO WA MUNGU.

To receive more information on how you can grow as a Christian, please get in touch with us on

**UK: +44 3333 448 612 / USA +1 240 781 6942**
**RSA +27 51 004 0209**

www.uebertangel.org | www.goodnewsworld.com

# AYA YA MAANDIKO KWA AJILI YA ULINZI

## ISAYA 54:

**14** NIMEJENGWA IMARA, NIKATHIBITIKA KATIKA HAKI. MBALI NA SHIDA YOY-OTE--HAKUNA CHA KUOGOPA! MBALI NA HOFU-_HATA HAITANIKARIBIA!

**15** MTU YEYOTE AKINISHAMBULIA, HATA SITAFIKIRI KWAMBA MUNGU AMEMTUMA. NA IKIWA YEYOTE ATANISHAMBULIA, HAKUNA LITALOTOKEA.

**16** MUNGU ALIMUUMBA MUHUNZI AFUKU-TAYE MOTO WA MAKAA NA KUFUA SILAHA ILIYOUNDWA ILI KUUA. PIA ALIMUUMBA MUHARIBU.

**17** LAKINI HAKUNA SILAHA INAYOWEZA KUNIDHURU AMBAYO IMEWAHI KUUNDWA. YEYOTE ATAKAYENITUHUMU ATAONDOLE-WA KUWA NI MUONGO. MIMI NI MTUMISHI WA MUNGU HIVYO NDIYO NINAYOWEZA KUTARAJIA MUNGU KWAMBA ATAONA ILI KUHAKIKISHA KILA KITU KINAFANYA KAZI KWA AJILI YA MEMA YANGU.

**HIKI NDICHO MUNGU ANASEMA KWANGU NA HAKITASHINDWA KWA JINA LA YESU!**

TRANSLATED FROM THE MESSAGE BIBLE IN ENGLISH

SUBSCRIBE

# SUBSCRIBE TO OUR YOUTUBE CHANNEL



**GoodNews Daily Devotional**
1,045,342 views

36K 0K



**GoodNews Daily Devotional**
100K Subscribers

Subscribed

Like Comment Share

SCAN ME

GoodNews Daily Devotional

@goodnewsdailydevotional

**TheGoodNewsWorld Helplines**

USA: +1 (240) 781-6942

UK: +44 333 344 8612

RSA: +27 (51) 004-0209

www.goodnewsworld.com